# Nipashe

Jumamosi Oktoba 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581099

The Guardian digital

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,039,594,915

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mbaroni** tuhuma kujifanya Ofisa Usalama Taifa uchaguzi CCM

UKURASA 2



GENEVIEVE UKWELI HUWA MCHUNGU

UKURASA 16

# Mashine ya kumulika hadi utumbo yaletwa kunasa dawa kulevya

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Philip Isdor Mpango, viongozi wengine wa Chama, Serikali, pamoja na Waumini wa Kanisa Katoliki, wakiwa kwenye misa takatifu ya kumuombea Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika Kanisa Kuu Katoliki, Jimbo la Bukoba, mkoani Kagera jana. **PICHA: IKULU**

## NECTA yachunguza mtahiniwa kuhujumiwa

UKURASA 3

# Rais Samia aagiza uchunguzi madudu miradi ya maendeleo

• **Ni** yale yaliyobainika mbio za mwenge, aziwashia moto TAKUKURU na ZAECA... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **YANGA YAFUNGUKA AL HILAL HAWAPONI** UK.32 **KABWELA** UK.7



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Kiongozi wa mbio hizo Kitaifa, Sahil Geraruma, katika Maadhimisho ya Kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru ambayo yalifanyika Kitaifa kwenye uwanja wa Kaitaba, mjini Bukoba, mkoani Kagera jana. **PICHA: IKULU**

# Samia ataka uchunguzi madudu miradi maendeleo

**Na Vitus Audax,** BUKOBA

RAIS Samia ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na ile ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kuchunguza miradi 65 yenye thamani ya Sh. Bilioni 12.8 iliyobainika kuwa na dosari wakati wa mbio za mwenge.

Samia alitoa maagizo hayo jana katika sherehe za kilele cha Mbio za mwenge zilizoambatana na kumbukizi ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, zilizofanyika mjini hapa.

Licha ya kutoa maagizo hayo, alizitaka taasisi hizo kujichunguza kwanza kabla ya kutekeleza kazi hiyo. Alisema taasisi hizo zimekuwa zikisubiri taarifa ya wadhibiti na wakaguzi wakuu wa hesabu za serikali na ripoti ya mbio za mwenge, hivyo kushindwa kufanya majukumu hayo kabla ili kubaini ubadhirifu ndani ya miradi hiyo.

"Kama taifa bado linatafunwa na vitendo vya rushwa, inasikitisha kuona kuna watu wasiojali hali za Watanzania kwa kutoa tenda kwa makandarasi wasio na uwezo. Viongozi tunaona ila tunasubiri vijana wakimbiza mwenge kuja kuvibaini. TAKUKURU na ZAECA toeni boriti katika macho yenu ili mvione vibanzi katika mboni za wengine. Hatuwezi kuendelea kusikiliza taarifa hizi hizi kila mwaka," alisema

Pia aliwataka wananchi na sekta ya afya kuzidisha mapambano dhidi ya malaria, ugonjwa ambao maambukizi yake yameshuka ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa UKIMWI ili kutokomeza maradhi hayo nchini.

Aliongeza serikali kwa sasa inapoteza kiasi kikubwa cha fedha katika kufanya matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na kupoteza nguvu kazi ya taifa kutokana na vijana wengi kujihusisha na matumizi ya dawa hizo.

Kuhusu Ebola, Rais Samia aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari na kujikinga na ugonjwa huo ambao mpaka sasa hakuna tukio lililoripotiwa nchini licha ya kuripotiwa kuwapo nchi jirani ya Uganda.

Awali, akiwasilisha taarifa ya mbio za Mwenge wa Uhuru, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema licha ya mafanikio ya mbio hizo, mwenge umegundua ubadhirifu katika baadhi ya miradi ya maendeleo.

"Mwenge wa Uhuru umezunguka kilomita 39,273.9 kuanzia Aprili 2, mwaka huu, katika mikoa 31 na halmashauri 195 ndani ya siku 195, ukitembelea, kuzindua na kuweka mawe ya msingi katika miradi 1,293 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 650," alisema.

Licha ya kuzindua miradi hiyo, miradi 65 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 12.8 ilitiliwa shaka na kutokuzinduliwa katika halmashauri 43 huku TAKUKURU ikiachiwa nafasi kuzifanyia uchunguzi.

Akisoma risala juu ya mwenendo wa ukaguzi uliofanywa na Mwenge wa Uhuru, kiongozi wa mbio hizo kitaifa, Sahili Neraruma, alisema Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unashindwa kuwafikia kimikopo kutokana na ubadhirifu wa baadhi ya halmashauri.

"Ukaguzi wa mbio za mwenge umebaini kuwa asilimia kubwa ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya vijana zimekuwa zikibanwa na baadhi ya halmashauri nchini huku zingine zikibadilishiwa matumizi na kutokusimamiwa vyema na TAMISEMI (Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) na kuwafanya vijana kukosa mikopo hiyo," alisema Gararuma.

Alisema vijana wanakopeshwa fedha hizo na kuzirejesha kwa wakati ili kuendeleza mzunguko wa ukopeshaji katika mfuko wa maendeleo ya vijana lakini halmashauri zimekuwa zinabadilisha matumizi yake na kukwamisha maendeleo ya mfuko huo.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema ndani ya mkoa wa Kagera, Mwenge huo umetembelea na kuzindua miradi 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 13.6 ikiwamo ya elimu, maji na barabara.

Chalamila alisema kwa sasa wananchi wa mkoa huo hawana dalili zozote za ubishani katika shughuli za kimaendeleo bali wanaendelea kutenda kazi na kuunga mkono juhudi za serikali.

## Mbaroni kwa tuhuma kujifanya Usalama wa Taifa uchaguzi CCM

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa linamshikilia Gabriel Kaserikali (34), mkazi wa Mbezi Mwisho mkoani Dar es Salaam, kwa tuhuma za kujitambulisha kwa baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Iringa Mjini kuwa ni Ofisa Usalama wa Taifa na kutoa maelekezo ya nani achaguliwe katika uchaguzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi alisema jana kuwa Oktoba Mosi mwaka huu, mtuhumiwa huyo alijitambulisha kwa wajumbe hao kuwa ni Ofisa Usalama wa Taifa kutoka Makao Makuu jijini Dodoma.

Alisema, mtuhumiwa huyo alijitambulisha hivyo baada ya kufika katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa (Iringa Girls) iliyoko Kata ya Kihesa, Manispaa ya Iringa walikokuwa wajumbe hao.

Kamanda Bukumbi alisema kuwa baada ya mtuhumiwa huyo kufanya hivyo, aliwaelekeza wajumbe hao wamchague mgombea Leonard Mgina, kwenye nafasi ya uenyekiti Wilaya ya Iringa Mjini, akidai ni maelekezo kutoka mamlaka ya juu serikalini.

"Jeshi la Polisi limefanya uchunguzi na kubaini kuwa mtuhumiwa huyu siyo mtumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na gari alilokamatwa nalo aina ya VW TOURAGE lenye namba za usajili T 858 DVE rangi nyeusi, amemtapeli Mohammed Nassoro ambaye ni mfanyabiashara wa magari wa Magomeni mkoani Dar es Salaam," alisema.

Kamanda Bukumbi alisema mtuhumiwa huyo alichukua gari hilo akijitambulisha ni mtumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na kupewa kwa makubaliano ya kufanya malipo ya awamu ya jumla ya Sh. milioni 18.5 lakini hakulipa kiasi chochote na kutoweka nalo.

Alisema, mtuhumiwa huyo amefikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Katika tukio lingine, Jeshi la Polisi mkoani humo limekamata mtambo (wheel loader caterpillar) wenye namba T 322 CAF, mali ya kampuni ya DB Shapriya & Co. Ltd ambao thamani yake ni Sh. milioni 250.

Kamanda Bukumbi alisema, katika tukio hilo wanamshikilia fundi, mkazi wa Nduli Manispaa ya Iringa mwenye umri wa miaka 42 ambaye jina limehifadhiwa, kwa tuhuma za kukutwa na mali za wizi zilizofunguliwa kwenye mtambo huo.

Alisema, tukio hilo lilitokea Oktoba 3 mwaka huu katika Kijiji cha Igingilanyi, Kata ya Isimani wilayani humo ambapo mtuhumiwa huyo inadaiwa alikutwa na vifaa mbalimbali vinavyodaiwa kutolewa kwenye mtambo huo ambavyo ni injini model no. 3126, rejeta moja, madgaurd nne, hydrolic pipe, wiring system, feni guard na propeller shaft.

# Watumishi h'shauri wafukuzwa kazi kisa ubadhirifu milioni 300/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WATUMISHI sita, wakiwamo Ofisa Biashara wa Wilaya ya Iramba na Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, wamefukuzwa kazi baada ya kubainika kuhusika katika ubadhirifu wa fedha za makusanyo ya mapato zaidi ya Sh. milioni 300.

Watumishi waliofukuzwa kazi ni kati ya 72 waliofikishwa katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhojiwa baada ya kubainika walizikusanya fedha hizo kutoka kwa wananchi lakini hawakuzipeleka benki kwenye akaunti za halmashauri.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kufuatia tuhuma dhidi ya serikali ya wilaya kushindwa kuchukua hatua dhidi ya wabadhirifu wa fedha za umma.

"Agosti 3, 2022 Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya Iramba lilikutana na kujiridhisha kuwa watumishi sita walikusanya fedha wakazitumia, hivyo likaazimia kuwafuta kazi akiwamo Ofisa Biashara wa Wilaya, Prosper Banzi na Mweka Hazina wa Halmashauri, Mwidin Mohammed," alisema.

Mwenda alisema, sio kweli kwamba serikali ya wilaya hiyo haijachukua hatua kwa wafujaji wa fedha, bali hatua zilianza kuchukuliwa haraka baada tu ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kutoa maagizo alipofanya ziara Julai 16 mwaka huu wilayani Iramba.

Alisema kuwa baada ya maagizo ya Waziri Mkuu, watumishi 72 waliogundulika walikusanya fedha pasi na kuziwasilisha katika akaunti ya halmashauri, walifikishwa TAKUKURU kwa ajili ya uchunguzi na hatua kuchukuliwa.

"Hadi hivi sasa ninavyoongea na ninyi, watumishi 49 ambao kati ya 72 waliofikisha TAKUKURU wameshalipa madeni yao jumla ya Sh. milioni 93 na wengine 11 walipewa siku 45 kuhakikisha wanarejesha fedha wanazodaiwa wasipofanya hivyo nao watafukuzwa kazi," alisema.

Mwenda alisema kuwa kabla ya kuanza uchunguzi wa suala hilo, aliagiza watumishi 18 wa halmashauri wasimamishwe kazi ili kupisha uchunguzi na watakaobainika hawakuhusika na ubadhirifu huo watarejeshwa kazini.

Aliongeza uchunguzi wa suala hilo unaendelea, akidokeza kuwa wapo watumishi wanaotoa hoja za utetezi pia wapo ambao waliomba muda ili waendelee kurejesha fedha.

Mwenda alisema malalamiko kwa waliokumbwa na hatua zilizochukuliwa na serikali ni lazima yawapo kwa sababu hawakutegemea kama hatua kali zingechukuliwa dhidi yao na sasa wanatumia baadhi ya vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii kupotosha ukweli makusudi.

Jumatatu wiki hii, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alitoa wiki moja kwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba waliofuja Sh. milioni 365 za makusanyo ya mapato wazirejeshe.

Serukamba, aliyezuru katika wilaya hiyo, alisema kama zikipita siku hizo na hawajarejesha fedha hizo, wahusika wote watafikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

# Jaji Mkuu ataka taarifa za wanaokiuka maadili

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amezitaka Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya kutoa taarifa kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama maadili yanayokiukwa na watumishi ili kuijengea mahakama imani kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi alipofungua mkutano kati ya Tume ya Utumishi wa Mahakama na watumishi wa mahakama pamoja na kupokea taarifa ya utendaji kazi wa Kamati za Maadili za Mkoa wa Singida.

Prof. Juma ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, alisema suala la maadili kwa watumishi wa mahakama linapewa kipaumbele na tume ili wananchi waendelee kuwa na imani na chombo hicho.

"Kamati zenu ni kama macho na masikio kusaidia kujua hali ya maadili kwa watumishi wa mahakama katika ngazi za mkoa na wilaya, ni mfumo shirikishi," alisema.

Jaji Mkuu alisema tume pekee yake haiwezi kufikia malengo yake ya kusimamia maadili ya watumishi wa mahakama bila msaada wa kamati za maadili ambazo zipo karibu na watumishi wa mahakama.

"Mpo katika nafasi nzuri kuifikishia tume taarifa zozote kuhusu masuala ya maadili, tume inawajali ninyi wenyeviti na wajumbe wa kamati kwani mnatusaidia kujenga imani ya wananchi kwa mfumo wa utoaji haki," alisema.

Prof. Juma alisema kamati zinazofanya kazi vizuri zinasaidia kuwajengea wananchi waachane na tabia ya kutoa tuhuma kwa hisia.

"Mara nyingi tumezoea kusikia mahakamani kuna tatizo la maadili, polisi kuna tatizo la maadili lakini tunawaambia wananchi wasihukumu watumishi wa mahakama kwa hisia, hivyo kama kuna kitendo kimefanywa na watumishi kipelekwe kwenye kamati," alisema.

Jaji Mkuu alisema mahakama imeendelea kuboresha utendaji wake kwa kufuatilia utendaji kazi kiteknolojia ambapo kila kazi inayofanywa na hakimu au jaji inafuatiliwa na hii inasaidia kupunguza malalamiko ya wananchi.

Aliongeza kuwa tatizo la rushwa lilikuwa likilalamikiwa katika mahakama na baadhi ya maeneo, lakini sasa nakala ya hukumu inapatikana kwenye mtandao na hivyo maboresho yanayoendelea kufanywa yanajibu hoja zinazotoka kwa wananchi.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Doroth Mwaluko, akitoa taarifa ya utendaji kazi wa Kamati za Maadili Mkoa wa Singida, alisema vikao vyote vya kamati vilivyofanyika ndani ya wilaya na mkoa havikuwa na malalamiko kuhusu mahakimu waliokiuka maadili ya kazi.

Mwaluko alisema, dosari iliyopo ni kwamba kamati zimekuwa zikipokea malalamiko kuhusu utoaji haki ambayo sio majukumu ya kamati pia wananchi wengi hawana uelewa kuhusu Kamati za Maadili.

# NECTA yachunguza mtahiniwa kuhujumiwa

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani (NECTA), limesema linaifanyia kazi taarifa iliyotolewa na mtahiniwa wa darasa la saba, Iptisum Slim wa Shule ya Msingi ya Chalinze Modern Islamic Pre and Primary School aliyedai kuwa alibadilishiwa namba ya mtihani wakati wa kufanya mitihani.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya taarifa hiyo juzi kusambaa katika mitandao ya kijamii video fupi ya mtahiniwa huyo akidai kuwa wakati wa mtihani huo, alipewa namba ya mtihani ambayo sio yake tofauti na alifanya kwa namba yake mtihani wa somo moja tu kati ya sita aliyofanya.

Kutokana na malalamiko hayo, taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari na Uhusiano wa NECTA, John Nchimbi, ilibainisha baraza limeona taarifa hizo kwenye mitandao ya kijamii na linazifanyia kazi.

"Baraza limeona taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimwonyesha mtahiniwa Iptisum Suleiman Slim, akisema kwamba alibadilishiwa namba yake ya mtihani wakati wa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE). Baraza la Mitihani linaifanyia kazi taarifa hiyo kuhakikisha mtahiniwa huyo anapata haki yake," Nchimbi alibainisha katika taarifa yake hiyo.

Katika video hiyo, Slim anadai kuwa siku ya mtihani huo, alipoingia darasani alipangiwa namba 40 wakati karatasi ya kutia saini ilipopita aliona jina lake lipo namba 39 na ndipo alipomjulisha msimamizi.

"Msimamizi alisema suala hili atalipeleka NECTA likarekebishwe. Hivyo, mitihani yote mitano niliifanya kwa namba 40 na mtihani wa sita ulipofika wakasema tubadilishane, hivyo nikaenda kwenye namba yangu halisi 39 na kufanyia mtihani wa Social Studies (Maarifa ya Jamii)," alidai.

Mtahiniwa huyo anadai kuwa baada ya kumaliza mitihani hiyo, baadhi ya wanafunzi, yeye akiwamo, waliitwa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo na kuwataka kukifanya kuwa siri kilichotokea wakati wa mtihani huo, akimnukuu "kisisikike sehemu yoyote wala tusiwaeleze wazazi".

"Ombi langu kwa Baraza la Mtihani ninaomba msaada nisaidiwe kisheria, Waziri wa Elimu , maofisa elimu watangazaji (waandishi wa habari) pia mnisaidie kupaza sauti yangu nipate haki yangu, yaani majibu yangu yarudi kwenye namba yangu, kwa sababu mtoto aliyenifanyia mtihani alikuwa anashika nafasi za chini na nilikuwa ninashika nafasi za juu 10 bora na mtihani wa majaribio ya mwisho ngazi ya wilaya nilishika nafasi ya kwanza," anadai.

Mtihani huo ambao ulifanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 5 mwaka huu, ulitarajiwa kujumuisha watahiniwa 1,132,084 wa shule za msingi waliosajiliwa kuufanya wakiwamo wasichana 584,614 sawa na asilimia 51.64 na wavulana 547,470 sawa na asilimia 48.36.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. …./20…**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HADIJA RAJABU MUYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWAJUMA JUMANNE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 08 Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 11 Mwezi 10 Mwaka 2022



**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**LUCAS WILLIAM MEVASHI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **T698 BRF ,** CHASSIS NAMBA: **1FPCJ707BB001513** na ENGINE NAMBA: **156FM12B5023002.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/403656/2022**

# Mashine ya kumulika hadi utumbo yanunuliwa kuzuia dawa za kulevya

- Bosi aanika siri kuwa na mahabusu yao
- Aitaja bangi mtihani mgumu kiutendaji

**Na Mary Geofrey,** BUKOBA

MAMLAKA ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA) imesema inaendelea na jitihada za kudhibiti dawa za kulevya zinazoingia nchini kupitia viwanja vya ndege na maeneo ya bahari.

Imebainisha kuwa moja ya hatua muhimu ilizozichukua ni kununua mashine ya X-Ray inayoweza kumulika hadi chakula alichokula mtu tumboni na begi zima katika viwanja vya ndege ikiwa ni jitihada za kudhibiti uingiaji wa dawa za kulevya nchini.

Kamishna wa Dawa za Kulevya nchini, Gerald Kusaya (Pichani) alibabinisha hayo katika mazungumzo yake na waandishi wa habari mjini hapa juzi kuhusu mikakati ya mamlaka hiyo katika kupambana na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Alisema hali ya udhibiti wa dawa hizo imekuwa kubwa zaidi katika maeneo kuingia nchini ikiwamo viwanja vya ndege ambako wasafirishaji hupitia kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Alisema katika viwanja vya ndege, kwa sasa hakuna mtu anaweza kupita na dawa za kulevya akasalimika kwa sababu wana mashine hizo zenye uwezo wa kuona kila kitu.

"Aliyemeza dawa za kulevya au kuweka kwenye begi hawezi kusalimika kwenye viwanja vyetu vya ndege," alisisitiza Kusaya.

Alifafanua kuwa kwa upande wa bahari, kutoka Tanga hadi Mtwara wanaendeleza doria kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Alisema, Zanzibar wanaendelea na doria katika maeneo yote ya mwambao wa bahari na Tanzania Bara wameboresha ulinzi katika kuhakikisha dawa hazitoki nje ya nchi kuingia nchini.

"Tumedhibiti dawa za nje kuingia nchini lakini za ndani zinaendelea kwa sababu bangi na mirungi zinazalishwa hapa, lakini zaidi ni bangi ingawa tunaendelea na operesheni za kudhibiti kwa kuwakamata watuhumiwa," alisema Kusaya.

Kamishna huyo alisema taarifa ya matukio ya udhibiti wa dawa za kulevya kwa miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba, zinaonyesha walikamata watuhumiwa wa dawa za kulevya 2,397.

Alibainisha kuwa kati yao, 29 ni wa dawa za kulevya aina ya Cocaine, 179 walikutwa na Heroine, watuhumiwa 1,934 wa bangi na watuhumiwa 244 wa mirungi.

Alisema kuwa katika kipindi hicho, waliangamiza mashamba 21 ya bangi na kuteketeza kilogramu 11,766. 88 za dawa za kulevya.

Alisema bangi peke yake waliteketeza kilogramu 6,680.44 kwa sababu ndiyo dawa za kulevya zilizopo kwa wingi nchini.




Aliongeza idadi hiyo pia inajumuisha kilogramu 22.66 Heroine, kilogramu 366 za Cocaine na kilogramu 4397.79 za mirungi.

"Katika kupambana na bangi, tunategemea zaidi wananchi watupe taarifa kwa sababu ndio wanaishi kwenye jamii ingawa nasi tunaendelea na operesheni zetu kila siku katika kuhakikisha tunamaliza tatizo hili nchini," alisema.

Kusaya alisema mwitikio wa jamii nao ni mzuri na wanatarajia kumaliza tatizo hilo endapo wananchi wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha.

**KWANINI VIJANA?**

Kamishna Kusaya alisema wameshiriki maonyesho ya vijana mkoani Kagera ili kutoa elimu kwa umma kama lilivyo lengo la mamlaka hiyo katika kupambana na dawa za kulevya.

Alisema wakishatoa elimu kwa jamii, watu wakielemika inakuwa rahisi kuepuka matumizi ya dawa za kulevya na kuwa mabalozi wazuri wa kuepuka matumizi hayo.

"Tumeshiriki maonyesho haya ya vijana kwa sababu vijana ndilo kundi kubwa linaloathirika zaidi na dawa za kulevya. Hata ukiangalia takwimu zetu tulizo nazo, kundi kubwa linaloathiriwa ni vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 40," alisema Kusaya.

Alisema hiyo ni fursa kubwa kwao kueleza vijana kwa upana hasara za dawa za kulevya na namna ya kuepuka matumizi hayo.

"Ninyi (waandishi wa habari) ni mashahidi kuwa vijana wanakuwa lakini hawafahamu mmea wa bangi umefananaje, ndio maana tumekuja nao tuwaonyeshe, inaweza kuwa kuna wengine wanakutana nao kwenye mazingira ya kila siku lakini hawajui kama ni bangi," alisema Kusaya.

**MAKUNDI YA DAWA**

Kusaya alisema yapo makundi mbalimbali ya dawa za kulevya zikiwamo zinazotoka nje ambazo ni Cocaine na Hetoine na Merthamane zinazotoka na uchanganyaji wa kemikali bashirifu.

Alisema nchini dawa za kulevya zilizopo ni bangi na mirungi ambazo ni kundi kubwa la dawa za kulevya zinazowasumbua.

Alisema, kundi la tatu ni dawa za binadamu 'tramadone' zenye asili ya kulevya ambazo watu wanazitumia kwa nia ovu - kwamba badala ya kuwa tiba, wanazidisha matumizi kuwa kilevi.

"Katika yote hayo ndio sababu tunakaa na vijana na kuwaonyesha yote na sheria yetu Na, 5 ya mwaka 2015 kwamba mtu anaweza kujiuliza kwanini tunashiriki maonyesho?

"Lengo kubwa ni kutoa elimu kwa sababu jamii ikielemika itachukia dawa za kulevya na kupunguza matumizi. Siku moja tuwe na Tanzania huru na hili linawezekana" alisema.

Alifafanua zaidi kuwa wametoa mwongozo wa kufundisha wanafunzi vyuoni na shuleni ili kujengewa uwezo namna ya kujikinga na matumizi hayo.

"Mwongozo upo, tunachofanya ni kuandaa walimu ili tupate wa kufundisha katika maeneo mbalimbali nchini. Peke yetu hatuwezi kusema kuwa tunaweza kufanya mapambano, ni jukumu la Watanzania wote," alisema.

Kusaya alisema vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika mapambano hayo ya kudhibiti dawa za kulevya kwa kutoa elimu kwa watu wengi zaidi.

**MADHARA YAKE**

Kusaya alisema yapo madhara yatokanayo na dawa za kevya ikiwamo kuvurugika kwa afya ya akili, saratani ya viungo vya mwili kama mapafu, maini na moyo.

Alisema, dawa hizo pia zinaathiri uzazi kwa wanaume ambao wanakuwa na uwezo hafifu wa kupata watoto na wanawake wanakuwa na uwezo hafifu wa kutunga mimba.

"Sasa tukienda namna hiyo, tutafika kwenye kizazi ambacho Watanzania tunazidi kupungua au tunakuwa na watoto ambao nao wameathiriwa na dawa za kulevya kutokana na wanachotumia wazazi wao," alionya.

Alisema, mamlaka inafanya kazi usiku na mchana kupambana na matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kuhakikisha Tanzania inakuwa huru isiyo na matumizi ya dawa za kulevya.

**BANGI TISHIO**

Kusaya alisema wanashirikiana na viongozi wa mashina, vitongoji na vijiji katika kupambana na uzalishaji wa bangi nchini.

Alisema bangi nyingi inalimwa kwenye maeneo yalikojificha na ndio sababu wanahitaji jamii kuwapa ushirikiano kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu.

Alisema kikwazo ni viongozi hao wa ngazi ya jamii kuwa sehemu ya wakulima au wamiliki wa mashamba hayo ya bangi, hali ambayo inakwamisha juhudi hizo za serikali ingawa mapambano yanaendelea.

Alitolea mfano walikwenda wilayani Kilosa mkoani Morogoro, kuangamiza shamba la bangi, lakini umbali wa kutembea kwa miguu ni saa nane kulifikia baada ya kushuka kwenye magari yao.

"Ukifika uliteketeze, ujitwishe sampuli na uhakikishe usiku haukukuti huko njiani ili urudi usije ukakutana na wahalifu kwa sababu ushawapatia hasara, wanaweza kukuvizia na kuwachoma kwa mishale yenye sumu au kuwadhuru kwa njia nyingine," alisema Kusaya.

**MAHABUSU YAO**

Alisema marekebisho ya sheria yaliyofanywa na Bunge ni kuhakikisha wanarekebisha vifungu ambavyo vilikuwa havipo sawa na kwamba sasa wanasubiri Rais Samia Suluhu Hassan, aipitishe ili kuwa sheria kamili.

Alisema, lengo la kuanzisha mahabusu zao ni kupata vielelezo vya kutosha kutoka kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya.

Alisema mahabusu hizo zitakuwa na vyoo maalum vya kujisaidia watuhumiwa hao ili kupata kete walizomeza kupitia vinyesi wanavyomeza.

"Mahabusu za kawaida hazina vyoo rafiki vya kupata vilelezo ndio sababu ya kuanzisha hizi za mamlaka ili kuendelea kukaa nao na kupata kama kuna dawa wamezimeza lakini hizi vilelezo vinapotea katika mazingira hayo," alisema.

Afafanua kuwa watazianzisha katika maeneo ambako kuna viwanja vikuu vya ndege kutoka nje kama Kilimanjaro, Dar es Salaam na Zanzibar, ambazo zitapokea pia wahalifu wengine kutoka kwenye vyombo vya dola.

"Kazi yetu kuwa itakuwa kuzihudumia na hazitakuwa zetu sisi bali na serikali na vyombo vingine vya dola vyenye watuhumiwa watawaleta," alisema Kusaya.

**SHISHA, GUNDI**

Kusaya alisema kwa sasa kuna makundi mengi ya dawa za kulevya ambazo zinatumiwa na watu ikiwamo gundi, shisha, petroli na ugoro ambayo hayapo kwenye kundi la dawa za kulevya.

Alisema jamii inatakiwa kusaidia kuondoa tatizo hilo kwa sababu wao hawawezi kukamata wanaotumia aina hiyo ya vilevi.

"Nikikuta mtu anatumia ugoro, siwezi kumkata ila nikimkuta anatumia shisha akichanganya na dawa za kulevya ndipo ninaweza kumkatamata, hivyo jamii inatakiwa itusaidie katika hili. Muda wote tupo tayari kufanya kazi, watupe taarifa, nasi tunalinda watoa taarifa wetu," alisema Kusaya.

**USULI**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ilianzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015. Sheria hiyo iliifuta Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kuanzishwa kwa Mamlaka Kulitokana na upungufu uliokuwapo katika mfumo wa udhibiti wa dawa za kulevya.

Upungufu huo ulikuwa ni pamoja na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliyoanzishwa na Sheria ya ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya Na. 9 ya mwaka 1995 kukosa nguvu ya kisheria ya kupeleleza, kufanya uchunguzi na kukamata wahalifu wa dawa za kulevya.

Kutokana na upungufu huo, Baraza la Mawaziri katika kikao chake cha tarehe 8 Novemba, 2007 (Waraka Na 60/2007) liliagiza kurekebisha au kufuta Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya Na. 9 ya Mwaka 1995, ili kukidhi matakwa na shida za udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Baraza la Mawaziri liliagiza kuundwa kwa chombo cha kupambana na dawa za kulevya chenye uwezo kiutendaji kwa kukipa mamlaka ya ukamataji, upekuzi na upelelezi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa dawa za kulevya nchini.

## Wafurahia kero ya maji kuondoka

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imemaliza tatizo la maji kwa wakazi wa Kata ya Mkuranga, mkoani Pwani lililodumu kwa kipindi kirefu.

Wakazi walionufaika na mradi wa maji ni zaidi ya 2,400 kati ya 6,000 wa mitaa ya Mipeko Center, Kibangulile, CCM, Ulega, Adili, Shule na Mtaa wa Mipeko B.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mipeko, Hamisi Mpili, aliipongeza mamlaka kwa kukamilisha mradi wa maji wa Mipeko unaotoa huduma katika maeneo yote ya kata ya Mkuranga.

Alisema shida ya maji Mipeko ilisababisha wananchi wa maeneo hayo kuhangaika usiku kutafuta huduma hiyo kwenye visima ambavyo si salama sana lakini kwa sasa wananchi wote wananufaika, hivyo kuipongeza serikali.

"Awali wananchi walitegemea maji ya visima vya asili na kipindi cha kiangazi visima vyote vinakauka, hivyo kusababisha shida kubwa kwa wanawake wanaoenda kutafuta huduma ya maji umbali mrefu zaidi na wakati mwingine usiku sana," alisema.

"Natoa rai kwa mamlaka wawe na vifaa vya kutosha. Wananchi wengi wanakuja kuchukua fomu za kutaka kuunganishiwa huduma ya maji katika ofisi zetu za serikali za mitaa ili wapate huduma ndani ya muda uliowekwa na DAWASA," alisema.

Naye Asha Zanda ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Mipeko, aliishukuru DAWASA kwa kufikisha huduma ya maji katika mtaa wao kwa kuwa imepunguza gharama ya maisha kwa wananchi wengi na huduma imekuwa karibu.

"Tunaishukuru serikali kupitia DAWASA, shida ya maji hapa Mipeko sasa ni historia. Zamani tulikuwa tunafuata maji mbali katika visima vya asili na kama vikikauka wakati wa kiangazi, ilitulazimu kununua maji kwa watu binafsi wenye visima vyao virefu ambapo tulinunua dumu kwa Sh. 500," alieleza.

Zanda alitoa wito kwa wakazi wa Mipeko na mitaa mingine waliopata huduma ya maji, kulipia huduma hiyo kwa wakati ili kuwezesha DAWASA kupata fedha za kuendeleza miradi katika maeneo mengine yasiyokuwa na huduma ya maji.

Awali, Msimamizi wa Mradi, Mhandisi Richard Katwiga, alisema utekelezaji wa mradi huo ulilenga kusogeza huduma kwa wananchi na chanzo cha maji cha mradi ni kisima cha maji kilichopo eneo la Mwanambaya chenye uwezo wa kuzalisha maji lita Sh. 50,000 kwa saa.

Alisema, mradi ulihusisha ulazaji wa bomba la inchi mbili na inchi 1.5 kwa umbali wa kilomita 2.5 na kwamba mradi ulikamilika Septemba na mpaka sasa zaidi ya wananchi 2,400 wananufaika na utekelezaji wa mradi huo.

"Natoa wito wangu kwa wananchi wanaopitiwa na mradi kuendelea kuleta maombi ya kuungiwa huduma ya maji na kulipia ili wafurahie huduma" alisema Mhandisi Richard Katwiga.

# Kliniki tembezi ya MOI yawatibu 400

**Na Mwanadishi wetu**

WAGONJWA 400 wamepata huduma za kibingwa za mifupa, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu katika kliniki jongefu ya MOI (MOI Mobile Clinic), iliyofanyika jana katika Hospitali ya Cardinal Rugambwa, Ukonga jijini Dar es Salaam.

Kliniki hiyo ni utekelezaji wa agizo la Wizara ya Afya la kuhakikisha huduma za kibingwa zinasogezwa karibu na wananchi.

Daktari Bingwa wa Mifupa MOI, Dk. Bryson Mcharo alisema mwitikio wa wakazi wa Gongo la Mboto umekuwa mkubwa na wagonjwa wote waliojitokeza wamepata huduma nzuri na kwa wakati.

Dk. Mcharo aliongeza kwamba asilimia kubwa ya wagonjwa waliojitokeza wana shida za mifupa na maumivu ya mgongo pamoja na magonjwa mengine.

"Leo (jana) tuko hapa katika Hospitali ya Cardinal Rugambwa tunatoa huduma kwa wakazi wa Gongo la Mboto na maeneo jirani kupitia kliniki yetu pendwa 'MOI Mobile Clinic', idadi ya wagonjwa waliojitokeza ni kubwa lakini wote wamehudumiwa," alisema Dk. Mcharo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Cardinal Rugambwa, Dk. Janerose Manyai aliushukuru uongozi wa MOI kwa kushirikiana na hospitali yake kuwahudumia wananchi na kuwapunguzia usumbufu wa kufuata huduma hizo MOI.

Mkazi wa Kitunda, Sophia Nestory aliishukuru MOI kwa kusogeza huduma karibu na hivyo taasisi zingine za afya ziige mfano huo kwa kuwa siyo watanzania wote wanaoweza kufuata huduma hizo MOI.




Mkufunzi na Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ilala, Mwinyimkuu Sangalaza (wa tatu kulia), akiendesha mafunzo ya uongozi kwa Wajumbe wa Baraza la Jumuiya ya Wazazi Kata ya Wazo, katika Ukumbi wa Bondeni Park Wazo Dar es Salaam juzi. Wengine ni Katibu wa EMMA Wilaya ya Kinondoni, Johnson Kashasha (kulia), Mwenezi wa CCM Kata ya Wazo, Hawa Mafumbi (wa pili kulia), Mwenyekiti wa CCM Kata Wazo, Abdallah Mbondela (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Wazazi Kata Wazo, Jesca Mrope. **PICHA: JOHN BADI**

# Bil. 1.7/- zatolewa ujenzi mabwawa kutibu majitaka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imeipatia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Singida (SUWASA) Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya kujenga mabwawa matatu ya kutibu majitaka ambayo uzalishaji wake umeongezeka na kufikia lita 12,803,519 kwa siku.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Sebastian Warioba alibainisha hayo jana wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa mabwawa hayo baina ya SUWASA na mkandarasi M/S Perntels Company and Nangai Engineering and Contractors Co.(T) Ltd na kushudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba.

Alisema kutokana na ongezeko la watu wanaofikia 193,116 katika Manispaa ya Singida, kumeshuhudiwa pia ongezeko la uhitaji wa maji linalofikia lita 15,063,048 kwa siku na hivyo kuwapo na ongezeko la uzalishaji wa majitaka.

"Majitaka yasipodhibitiwa kwa wakati yanaweza kusababisha athari za kiafya na kimazingira kwa wananchi, hivyo serikali imetoa Sh. bilioni 1.7 kujenga mabwawa ya kutibu majitaka na gari moja la kunyonya majitaka," alisema.

Warioba alisema fedha hizo zimetolewa baada ya SUWASA kusanifu mabwawa matatu ya kutibu majitaka katika Manispaa ya Singida yatakayosaidia kuboresha usafi wa mazingira.

Alisema mradi huo utakapokamilika utanufaisha wananchi 259,539, utaboresha usafi wa mazingira na afya kwa wananchi na kutatoa fursa ya kilimo cha mboga, matunda na miti kwa kuwa maji yatakayopatikana yatakidhi viwango vya kilimo cha umwagiliaji.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, aliagiza SUWASA kuhakikisha inamsimamia mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ili aikamilishe kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha.

Aliagiza SUWASA iweke mpango mkakati wa kuwa na mifumo ya ukusanyaji majitaka katika manispaa ili kuwa na mji wa kisasa ambao unakidhi mahitaji.

Serukamba pia aliagiza mamlaka hiyo kuongeza wigo wa mtandao wa huduma za maji hasa maeneo ya pembezoni mwa mji na pia wadau wawe wanalipa ankara za maji kila mwezi ili kuiwezesha SUWASA kumudu gharama za uendeshaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga, Azam FC hamjamaliza kazi Afrika

**WAWAKILISHI** wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba, Yanga na Azam FC, zote za Dar es Salaam wanatarajia kushuka kwenye viwanja tofauti kesho kwa ajili ya kupeperusha bendera ya nchi kusaka tiketi za kutinga hatua ya makundi.

Timu hizo zitashuka kucheza mechi za marudiano, Simba na Azam zikiwa nyumbani wakati Yanga wao wamesafiri kwenda Sudan kuwafuata wapinzani wao, Al Hilal.

Simba yenyewe itashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwakaribisha Premiero De Agosto kutoka Angola katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa, ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-1 waliyopata ugenini wiki iliyopita.

Ikiwa ugenini jijini Khartoum, Sudan, Yanga watawavaa wenyeji Al Hilal, wote wakiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1, Yanga ikianza kufunga na Waarabu hao wanaofundishwa na Mkongomani Florent Ibenge wakisawazisha.

Mwakilishi mwingine ni Azam FC, matajiri hao wa Chamazi wanatarajia kuwakaribisha Waarabu wa Libya, Al Khadar, mchezo utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Azam FC inayoongozwa na Kocha Mfaransa mwenye rekodi kubwa katika mchezo huo Afrika, yenyewe katika mechi yake ya kwanza iliyochezwa jijini Benghazi, ilikubali kichapo cha mabao 3-0.

Kwa upande wa Zanzibar, Kipanga FC kesho itakuwa ugenini kuwakabili Club Africaine katika mechi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikitoka sare ya bila kufungana walipokutana wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Kila timu inafahamu vyema imecheza dakika 90 za kwanza na sasa wanatakiwa kumaliza muda kama huo wa marudiano na hatimaye kupata mshindi wa jumla ambaye atasonga mbele kwa kutinga hatua ya makundi.

Kujituma, kupambana na kucheza kwa juhudi ndio jambo pekee linalosubiriwa kuonekana kutoka kwa wachezaji wa timu hizi nne kwa ajili ya kujitangaza vyema kimataifa.

Tunawakumbusha wachezaji wa timu zote hakuna ambaye anatakiwa kubweteka katika mechi za kesho kwa sababu mpira wa miguu kamwe hautabiriki na uamuzi wake hujulikana pale mwamuzi aliyepewa mamlaka atakapopuliza filimbi ya mwisho kuashiria amemaliza mchezo.

Simba inatakiwa kusahau ushindi walioupata Angola na kuingia uwanjani kwa malengo ya kusaka ushindi, hawa wanafahamu wanatavyotakiwa kupambana kwa sababu wanakumbuka kilichowakuta katika msimu uliopita ambapo walitolewa na Jwaneng Galaxy, ambayo ilifanikiwa kupindua meza kwa Mkapa.

Ili kuhakikisha aibu hii haijirudii, wachezaji wa Simba wanatakiwa kuamka na kusaka ushindi mapema, kwa kuanza kufunga bao kesho, itawaweka na itawachanganya wapinzani wao ambao wataona wameelemewa na mlima mrefu kurudisha magoli waliyofungwa lakini kwa upande wa Yanga wao watatakiwa kushuka dimbani wakiamini wanauweza wa kushinda ugenini.


Yanga inatakiwa ifahamu kama Al Hilal aliweza kupata bao, wao pia wanaweza kufunga ugenini na kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele, mpira wa sasa uko wazi, utulivu na kucheza kwa nidhamu ndio jambo ambalo litawasaidia kuwavusha kutoka hatua waliyopo na kusonga mbele katika michuano hiyo wanayoshiriki.

Simba na Yanga, endapo zitatolewa kwenye michuano hiyo ya juu kwa ngazi za klabu barani Afrika, zenyewe zitaangukia katika mechi za mtoano kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini Azam na Kipanga zitakuwa zimeyaaga mashindano hayo ya CAF kwa msimu huu.

Kwa sababu mpira umebakiza dakika 90, tunazikumbusha timu zote kupambana ili kuhakikisha wanashinda na hatimaye kwa upande wa Tanzania Bara, kuendelea kuzilinda nafasi nne za uwakilishi kwenye michuano hiyo.

Kila la kheri Simba, Yanga, Azam FC na Kipanga katika kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mashabiki kutumia Vuvuzela ni ushangiliaji wa kizamani

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara ya kwanza kwenye historia ya soka duniani, Afrika ilikuwa mwenyeji wa Kombe la Dunia mwaka 2010, ambalo lilichezwa Afrika Kusini na Hispania ikawa timu iliyojiwekea rekodi ya kulitwaa kombe hilo kwenye bara hili.

Kwenye michuano hiyo ilishuhudiwa kwa mara ya kwanza matumizi ya vifaa vya kupuliza ambavyo havitofautiani sana na matarumbeta, saxaphone, trombone na vifaa vingine vinavyofanana na hivyo.

Vifaa au vyombo vya kupuliza asili yake ni Afrika, na vilianza na pembe za wanyama, ambazo zilikuwa zinatobolewa kwa namna ambayo ilipulizwa inatoa mlio.

Karne na karne zilizopita ilikuwa inatumika kwenye muziki, na hata kupeana taarifa. Jinsi pembe inavyopulizwa tu, wananchi au wanakijiji wanajua mlio huo ni wito wa heri au shari au kuna vita.

Watu kutoka bara Ulaya walijiongeza kama kawaida yao na kutengeneza vifaa vingine kwa kutumia madini mbalimbali, plastiki au bati ambavyo navyo vilianza kutoa mlio kama wa ulio kwenye pembe za wanyama.

Huo ndiyo mwanzo wa kuwa na vyombo vya muziki wa kupuliza hivi tunavyoviona sasa, lakini vyote asilia yake ni pembe za wanyama.

Wakati wa fainali za Kombe la Dunia huko Afrika Kusini, Wasauzi walitengeneza vifaa vya kupuliza vya plastiki ambavyo waliviita Vuvuzela.

Walikuwa wakijazana uwanjani kila mmoja akiwa na cha kwake wakivipulizi na kutoa sauti ambayo uwanja mzima watu hawasikilizani. Ni sauti ambazo hata kama kuna watu wanaimba sauti haziwezi kusikika. Na hata wanaopiga vigoma nao pia hawasikiki.

Kwa utamaduni wa mpira wa miguu ni sehemu ambayo watu wanakwenda kufurahia, kucheza na kuimba ili kuwatia moyo wachezaji wao na upande wa pili kuwazodoa wapinzani wao.

Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), lilikiri kweli ni tatizo mavuvuzela kuwapo uwanjani na sauti zake zinakera masikioni kwa sababu zinapigwa nyingi kwa wakati mmoja, lakini iliruhusu zitumike Afrika Kusini kutokana na kuwa ni utamaduni wa huko.

Ndiyo maana haikushangaza baada ya hapo, bara la Ulaya na mengine yakapiga marufuku kutumia kwa sababu mbalimbali.

Wenzetu wanachotaka ni kuimba, ili ujumbe usikike vizuri kwa wachezaji wao kuliko kupulizia vitu ambavyo havina ujumbe wowote. Na pia sauti hizo zinakuwa hazina athari kwa wapinzani kwani wachezaji wa timu zote mbili wanasikia hicho hicho tu kinachosikika.

Ulaya utakuta mashabiki wanawaimba kwa majina wachezaji wao ili kuwapa nguvu ya kupambana kupata ushindi, hivyo kama wangeruhusu mavuvuzela kutumika sauti zisingesikika.

Nimeona na kusoma mahala mashabiki na wanachama na Simba wanahamasishana mashabiki wao kutokwenda na mavuvuzela uwanjani, badala yake wajazane na kuimba nyimbo mbalimbali kwa nguvu za kuwatia hamasa wachezaji wao na kuwatisha wapinzani.

Hii haina maana wote wasiende nayo, ila wawe wawili au watatu tu kwa ajili ya kunogesha nyimbo na si kama tunavyoshuhudia baadhi ya mechi kunakuwa na sauti za vuvuzela tu mwanzo hadi mwisho.

Mfano Simba kesho itacheza dhidi ya Primeiro de Agosto kutoka Angola, mashabiki wanatakiwa kushangilia kwa kuimba zaidi na ngoma kuliko vuvuzela. Sauti ziwafikie wachezaji wao wakiimbwa na kupewa moyo, lakini kelele za kutisha ziwe zinawafikia wapinzani na kujiona kweli wapo ugenini.

Tumeona katika mataifa yalioendelea kisoka na hata hapa Afrika, sauti za mashabiki ndiyo silaha kubwa za ushindi kwa timu zao.

Nadhani mashabiki wa Simba wanaweza kuwa mfano wa hilo na baada ya hapo kwa timu nyingine zifuate kwa sababu matumizi ya vuvuzela naona ni kama yamebaki Tanzania labda na nchi chache tu duniani, lakini kwenye nchi mbalimbali hata Afrika, mashabiki ndiyo wamekuwa wakishangilia kwa kuimba, kucheza na kupiga kelele za kushangilia au kuzomea kwa ajili ya kuipa faida timu yao, hasa ikiwa nyumbani.

Imefika wakati sasa mashabiki wawe wanapeleka ujumbe wa sauti zao kwa kuimba kwa sababu wachezaji wanapata hamasa zaidi kuliko vuvuzela.

## HABARI KITAIFA

### Jamii ya Hindu yajitosa mauaji

**Na Romana Mallya**

KUTOKANA na vitendo vya mauaji vinavyoendelea kuripotiwa nchini, Jamii ya Hindu inayoishi Tanzania, imewakumbusha wananchi kuwa binadamu wote ni sawa na hakuna aliye mkubwa wala mdogo.

Jijini Dar es Salaam juzi, mwakilishi wa jamii hiyo, Venkat Veda anayejitolea katika Taasisi ya Swayamsevak Sangh Organization (HSS), alitoa kauli hiyo wakati wa maadhimisho ya taasisi hiyo na sherehe ya Vijaya Dashmi (ushindi wa vizuri juu ya vibaya).

Vijaya Dashmi, ambayo pia inajulikana kama Dussera, ni kati ya sherehe muhimu na kubwa zaidi za Kihindu zinazoadhimishwa India kila mwaka na huadhimishwa Oktoba 10, siku ya mwezi wa kalenda ya Hindu ya Ashwin. "Kuanza kujiita mimi ni mkubwa kuliko huyu au mdogo kuliko huyu haileti maana, lazima uone binadamu wote ni sawa," Veda alisema.

"Hindu ni kufikiri na kuweka akili yako kwenye kitu unachokiona hakijaelezwa vizuri. Kwa hiyo, unakieleza vizuri, kukitafakari na kufanya mijadala," alisema.

Kuhusu amani na utulivu na matukio ya mauaji yanayoendelea kuripotiwa nchini, Veda alisema kama kila mtu akijitafakari, atabaini binadamu wote ni sawa, hivyo hakuna atakayempiga mwenzake.

"Ukishaanza kufikiri hivyo, huwezi kufikiria kumpiga mwenzako. Nikianza kujitafakari na wewe ukajitafakari unagundua binadamu wote ni sawa, kuanza kujiita mimi ni mkubwa kuliko huyu au mdogo kuliko huyu haileti maana.

"Kukosa amani au kukosa utulivu kunatokana na mtu kujifanya yeye ni mkubwa au anajua kuliko mwingine," alisema.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan ambaye alikuwa miongoni mwa washiriki, alisema, "Nimefurahi sana kuona Watanzania wameshiriki katika hafla hii iliyoandaliwa na Hindu Swayamsevak Sangh Tanzania."

Pradhan alisema HSS ipo nchini kwa miaka 12 sasa na ina wanachama mbalimbali wakiwamo Watanzania na imekuwa ikiwaleta pamoja kuzungumzia utamaduni wa India na thamani ya jamii hiyo na namna ya kuwaunganisha vijana na watoto.

Katibu Mkuu wa HSS, Shailesh Karyavah alisema: "Leo Wahindu wamekusanyika kusherehekea siku hii maalum ya kupigana na adui waliopo duniani katika sura ya kutafuta usawa."

Karyavah alisema kila Jumapili wamekuwa wakikutana kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na namna ya kuboresha utimamu wao wa mwili, kufanya mazoezi (yoga), kujadili kero zilizopo katika jamii na namna ya kusaidia kuziondoa

"Wiki ijayo tunatarajia kuandaa kambi ya wagonjwa wa kisukari wilayani Mkuranga ili kuruhusu watu kupima afya zao na tutaambatana na daktari kuwaelimisha kuhusu ugonjwa huu, vyakula vinavyotakiwa kuliwa kila siku na masuala mengine ya kumfanya mtu kuwa na afya bora," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Khadija Ali, akizungumza wakati akizindua kituo cha mafunzo ya ufundi cha Reach the Goal kwa ajili ya mabinti waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba na ndoa za utotoni kinachosimamiwa na mashirika ya Himiza Development Organization na Lutogo Development Initiative, eneo la Mwanambaya wilayani humo juzi. Kutoka (kulia) ni Mwanzilishi wa Lutogo, Lulu Mwalubandu, Mkurugenzi wa Himiza, Prisca Ngweshemi na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Timothy Kudra. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Yatakayojiri ziara ya siku tatu ya Majaliwa Mwanza

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajia kufanya ziara ya kikazi siku tatu mkoani Mwanza, ikilenga kukagua miradi ya kimkakati na kuzungumza na wananchi wa mkoa huo.

Ziara hiyo ya Waziri Mkuu inatarajiwa kuanza leo, Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni akianza na ukaguzi wa ujenzi wa Daraja la Magufuli, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na baadaye kuzindua jengo la huduma ya macho katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando.

Akizungumza na waandishi ofisini kwake jana, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima alisema kuwa Oktoba 17 mwaka huu, Majaliwa atakagua ujenzi wa Kituo cha Afya Ilugwa na ujenzi wa Shule ya Sekondari Ilugwa wilayani Ukerewe.

"Ziara ya Waziri Mkuu hapa Mwanza ni ya manufaa makubwa. Lengo ni kuhakikisha miradi ya maendeleo inakamilika kwa wakati, ili wananchi wanufaike na matunda yatokanayo na serikali," alisema.

Malima, alisema kuwa Oktoba 17, Waziri Mkuu atatembelea Kisiwa cha Ghana kwa lengo la kukagua ujenzi wa zahanati ambayo iko hatua ya msingi.

Alisema kuwa Waziri Mkuu pia atakagua ujenzi wa stendi ya Nyegezi iliyoko wilayani Nyamagana na baadaye atazungumza na wananchi wa eneo hilo kisha kwenda Bandari ya Mwanza Kusini kukagua miradi wa ujenzi wa Meli ya MV Mwanza.

Malima alisema mradi wa ujenzi wa meli hiyo ulikuwa ukisuasua na kwa sasa unaendelea vizuri na kutoa angalizo kwamba ujenzi wa mradi wa maji Ukerewe unapaswa kukamilika Novemba 15, mwaka huu, vinginevyo mkandarasi atawajibika.

## KABWELA



# Mzee mbaroni tuhuma za kunajisi mwanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia Abubakari Said (64), mkazi wa Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga kwa tuhuma za kumnajisi mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka 14 anayesoma katika Shule ya Sekondari Mazinge.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kumrubuni mwanafunzi huyo kwa kumpatia Sh. Sh. 10,000 kisha kumpeleka chumbani kwake na kuanza kumnajisi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Jackson Mwakagonda alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 10 mwaka huu majira ya saa nane mchana nyumbani kwa mzee huyo.

Mwakagoda, alidai mbinu aliyotumia mzee huyo kumnajisi mwanafunzi ni kumrubuni kwa kumpa Sh. 10,000, naye kuingia kwenye ukatili huo kwa kuingia chumbani kwa mzee huyo na kutendwa kitendo hicho.

Alisema, jeshi hilo linaendelea na upelelezi na ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Alitoa wito kwa wazazi na walimu kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi shuleni na kama hawako shuleni, wajiridhishe waliko ili kuzuia vitendo hivyo vya kufanyiwa ukatili.




Mbunge wa Viti Maalum kundi la Watu wenye Ulemavu, Stella Ikupa (katikati waliokaa), akikabidhi kitanda cha kujifungulia wajawazito wenye ulemavu kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. Deo Nyaga kilichotolewa kwa ufadhili wa Mgodi wa Barrick na Ikupa Trust Found, wilayani humo juzi. Wengine ni watumishi wa hospitali hiyo na mgodi huo. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mbunge: Kuwe na wodi za wajawazito wenye ulemavu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MBUNGE wa Viti Maalum anayewakilisha kundi la Watu Wenye Ulemavu, Stella Ikupa amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha wanatenga wodi katika hospitali za wilaya na vituo vya afya kwa ajili ya kujifungulia wajawazito wenye ulemavu.

Ikupa, alitoa rai hiyo jana alipokabidhi kitanda kwa ajili ya kujifungulia wajawazito wenye ulemavu na baskeli tano kwa watoto wenye ulemavu zenye thamani ya Sh. milioni 3.1 katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, vyote vikifadhiliwa wa Mgodi wa Barrick na Ikupa Trust Foundation.

Alisema kuwa wakati wa kujifungua, watu wenye ulemavu wanahitaji usiri mkubwa tofauti na makundi mengine kutokana na maumbile waliyonayo, hivyo siyo vyema kuchanganywa wodi moja na wajawazito wasiokuwa na ulemavu kwa kuwa hunyanyapaliwa pindi wakijifungua.

"Tukipata tu ujauzito jamii inatushangaa na kutuona watu wa ajabu kupata ujauzito huku tukiwa na ulemavu. Je, wakiona maumbile yetu wakati wa kujifungua huoni kama watatuona kituko, tunaomba kutengewa wodi ili tufiche maungo yetu," alisisitiza Ikupa.

Alisema suala la kuoa na kuolewa kwa watu wenye ulemavu pia linachukuliwa tofauti kwenye jamii na pale mtu anapooa au kuolewa na mwenye ulemavu, anachekwa na kuonekana hana maana.

Ikupa, alitoa wito kwa jamii kuacha tabia za kuwanyanyapaa watu wenye ulemavu kwa kuwa nao wana haki kama yalivyo makundi mengine katika jamii.

Mwenyekiti wa Idara ya Wanawake na Watu Wenye Ulemavu Manispaa ya Kahama, Rehema Joshua alisema kitanda cha kujifungulia walichopokea kitawasaidia kupata mazingira rafiki ya kujifungua.

Alisema, wajawazito wengi wenye ulemavu wanashindwa kujitokeza na kujifungulia vituoni kutokana na kuwapo mazingira ambayo siyo rafiki kwao ikiwamo kuchanganywa wodi moja na wajawazito wasiokuwa na ulemavu.

Awali akipokea msaada huo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. Deo Nyaga alisema wamekuwa wakipokea wateja wenye ulemavu mbalimbali na kuwahudumia kulingana na mazingira na vifaa vilivyopo, hivyo kupatikana kwa kitanda hicho kutaondoa baadhi ya adha hizo.

Alisema, suala la kutenga chumba kwa ajili ya wajawazito wenye ulemavu linashughulikiwa na uongozi kwa kuwa kuna jengo linaendelea kujengwa kwa ajili ya kinamama na watoto wadogo na wajawazito wenye ulemavu watapata wodi ndani ya jengo hilo.

Kaimu Meneja Uhusiano wa Jamii wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Zuwena Senkondo alisema wataendelea kushirikiana na serikali katika kuwapatia mahitaji watu wenye ulemavu ili kuhakikisha nao wanatimiza ndoto zao kama walivyo watu wengine.

## Kampuni yatoa hadhari utapeli

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kopafasta Microfinance Limited, imetoa ufafanuzi kuhusu taarifa iliyotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Oktoba 12, 2022 kuhusu utapeli unaofanywa na baadhi ya watu na kampuni kupitia mitandao.

Kampuni hiyo imesema tayari imewasilisha barua rasmi BRELA kuwaomba kuufahamisha umma kuhusu uhalali wa Kopafasta Microfinance Limited.

Meneja Mtendaji wa Kampuni ya Kopafasta Microfinance Limited, Patrick Kang'ombe aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa jina lililotajwa na BRELA ambalo ni 'Kopa Fasta Company Limited', halina uhusiano wowote na kampuni hiyo.

Alisema, kampuni yake ilisajiliwa kwa kuzingatia sheria kwa jina la 'KOPAFASTA MICROFINANCE LIMITED' na kupewa cheti cha usajili Na. 138564851 kilichotolewa na Msajili wa Kampuni – BRELA Agosti 9, 2019.


Kang'ombe alifafanua kuwa, Kopafasta Microfinance Limited inaisihi jamii kuepuka matapeli ambao wengi hutumia mitandao ya kijamii na kwamba wasikubali kulipa kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya kupata mkopo, mbinu ambayo ni maarufu na inayotumiwa na matapeli kujipatia fedha kwa kutumia majina batili yenye mfanano na majina halisi.

Alisema, "Mikopo inayotolewa na kampuni yetu hutumia vigezo vinavyozingatia sheria za nchi, hakuna anayepaswa kutoa fedha ili kupata mikopo hiyo na kupitia taarifa hii tunawasihi watanzania wanaohitaji kupata mikopo mbalimbali kupitia Kopafasta Microfinance Limited, kupiga simu kwa uongozi wa kampuni yetu.

"Lakini, unaweza kufika katika ofisi zetu zilizopo Barabara ya Garden, Mikocheni tafadhali, toa taarifa haraka kwa vyombo vya usalama unapobaini jaribio la utapeli," alishauri.

BRELA, kupitia taarifa yake iliyolenga kutoa ufafanuzi kuhusu kampuni ya Kalynda e-commerce Limited Oktoba 12, 2022, ilieleza: "Hivi karibuni kumekuwa na tabia ya watu wasio waaminifu kughushi vyeti vya kampuni, majina ya biashara na leseni za biashara kwa lengo ovu la kuwatapeli wananchi.

"Baadhi ya vyeti vilivyoghushiwa ni pamoja na Kopa Fasta Company Limited, Champion Investment na Africa. Taarifa zimeshatolewa kwenye vyombo vya dola kwa ajili ya hatua za kijinai."



## Shirika labuni utaratibu kuvutia unawaji mikono

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SHIRIKA la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wake wa ('WASH SDG Programme), limeanza mchakato wa kuweka alama za miguu zenye rangi za kuvutia kwenye vyoo, kikiwamo cha Kituo cha Mabasi Madogo cha Kilombero jijini Arusha, ili kuelekeza watumiaji wa vyoo hivyo eneo la kunawa mikono.

Akizungumza jana wakati wa uwekaji alama hizo, Mratibu wa Usafi wa Mazingira Mijini wa Mradi huo, Leyla Khalifa alisema wameamua kuleta mbinu inayotumiwa na meneo mbalimbali kwenye nchi zingine, yakiwamo ya viwanja vya ndege na kuweka alama kwenye stendi hiyo ili kubadilisha tabia za watu kuhusu unawaji wa mikono.

"Unawaji mikono ni muhimu hasa pale mtu anapotoka chooni, kwani inasaidia kuepusha wengine na magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu, UVIKO-19 na sasa Ebola ambayo ipo nchi jirani ya Uganda," alisema.

Alibainisha kuwa njia hiyo inasaidia hasa maeneo ya shule ambako wanafunzi wengi hupenda kufuata alama hizo za nyayo zinazoonyesha maeneo ya kunawa mikono kutokana na rangi zake na kujikuta wananawa mikono yao kila wanapotoka chooni.

Alisema kuwa anaamini alama hizo zikifanikisha kubadilisha watu tabia na zitasaidia Halmashauri ya Jiji la Arusha kusambaza alama hizo kwenye maeneo yenye watu wengi kama vituo vya afya, shuleni na sokoni ili kuhimiza kila mtu kunawa mikono.

"Watu wengi hujikuta wakiingia chooni na kujisaidia kisha kutoka bila kunawa mikono, hata kama anaona sabuni na maji, hivyo tumeamua kuja na kitu cha tofauti labda itasaidia kubadilisha tabia hizi za baadhi ya watu," alisema.

Kwa mujibu wa Leyla, wapo baadhi ya watu pia wanatumia maji vibaya kwa kufungulia bomba na hivyo kupoteza maji mengi na kuacha yakimwagika ovyo, kitu ambacho hakifai.

Pamoja na mambo mengine, alihimiza umuhimu wa kujali kuhusu matumizi kidogo ya maji, kulingana na mabadiliko ya tabianchi ambayo husababisha upungufu kwa maji.

"Wale wenye ndoo za kunawa mikono, ni vizuri wakatumia maji yaliotumika kunawa mikono na kumwagilia bustani badala ya kuyamwaga ovyo," alisisitiza.

Hata hivyo, kiongozi huyo hakueleza usalama wa maji hayo kutumika kumwagilia mazao ilhali yanakuwa na mchanganyiko wa kemikali zitokanazo na sabuni.

# DED amulika matumizi ya fedha ujenzi wa madarasa

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi amewaagiza maofisa wa serikali wanaosimamia mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 38 katika shule 15 za sekondari, kuzingatia kanuni, sheria na utaratibu wa matumizi ya fedha za umma.

Mradi wa ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa unaobatizwa jina la 'Pochi la Mama', unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 760 hadi kukamilika kwake.

Msumi aliagiza hayo juzi wakati wa kikao kazi maalum kilichokuwa na lengo la kukumbusha sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya serikali.

Msumi aliagiza wasimamizi hao kushirikiana kama timu katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi huo , akiwataka kufuata utaratibu wote, ukiwamo wa utunzaji wa taarifa zote muhimu pamoja na kuikamilisha mradi kwa wakati.

"Fedha zimeshaingia kwenye akaunti za shule, tunakwenda kujenga vyumba 38 vya madarasa kwa Sh. milioni 20 kwa darasa yakiwa na madawati 40 na utekelezaji utatumia nguvu kazi ya ndani (Force Account), pia utatumia ramani zilizotumika kwenye programu ya Lipa Kutokana na Matokeo 'EP4R' na ujenzi utakamilika ndani ya siku 75," aliagiza.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa Force Account na utashirikisha jamii kwenye ujenzi kwa kuwa ni wajibu wa kila mtu mwenye dhamana ya kusimamia na kushiriki kutekeleza majukumu hayo kwa ajili ya kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Mkuu wa Idara ya Mipango wa Halmashauri hiyo, Anna Urio alisema lengo la kikao hicho ni kukumbushana na kupata uelewa wa pamoja kuhusu utaratibu za matumizi ya fedha za serikali katika utekelezaji wa ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa.

"Kila mwenye dhamana anatakiwa kufahamu kiasi cha fedha na idadi ya madarasa, kadhalika muda wa utekelezaji kwa kuzingatia ubora wa mradi unaoendana na thamani ya fedha, pia ushirikishwaji wa jamii kwenye ujenzi wa miradi yote," alisema Ofisa Mipango Anna.

Mkuu wa Idara ya Ujenzi katika Halmashauri ya Arusha, Nuru Mkwazu aliahidi kuzingatia hatua za awali ikiwamo namna ya kupata makandarasi na wazabuni kupitia ushindani kwa kuzingatia bei halisi ya soko na gharama ya mradi na uteuzi wa kamati za usimamizi wa mradi.

Vilevile, Kaimu Mweka Hazina wa Halmashauri hiyo, Tido Moiro, alisema watahakikisha mkandarasi analipa kodi zote za serikali ikiwamo ya asilimia tano ya gharama ya mkataba fedha ambayo itazuiliwa mpaka kazi itakapokamilika na endapo itatokea tatizo lolote fedha hizo zitatumika.




Wafanyakazi wa Songas wakiwa pamoja na wanafunzi wenye ulemavu wa akili na viungo wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Jangwani, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, baada ya kutoa msaada wa viti vya magurudumu, taulo za kike na vifaa vya kujifunzia, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Afya ya Akili Duniani. Kushoto ni Meneja Maendeleo ya Kijamii wa Songas, Nicodemus Chipakapaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kampeni Kata kwa Kata kuundwa kukabili ukatili

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

KUPAA kwa takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia, mauaji yanayotokana na wivu wa mapenzi, migogoro ya ndoa na mimba za utotoni, kumeisukuma Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuja na mkakati kukabiliana nayo.

Wizara hiyo imejiapiza kuja na kampeni maalum ya Kata kwa Kata kutoa elimu ya namna ya kupambana na vitendo hivyo.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju alipokuwa Kijiji cha Mandi, Wilaya ya Babati mkoani Manyara, alikokwenda kufunga kampeni ya ukeketaji.

"Tuko tayari kwenda Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya, Tarafa kwa Tarafa, Kata kwa Kata, Kijiji kwa Kijiji, Kitongoji kwa Kitongoji na Kaya kwa Kaya ili kuhakikisha vitendo vya ukatili vinatokomezwa.


"Hiyo kampeni siyo ya wizara peke yake, itakuwa ya kila mtu, hivyo inabidi watu wote waiunge mkono. Lengo ni kuhakikisha vitendo vya ukeketaji na ukatili mwingine, vinatokomezwa na kumlinda mtoto, mwanamke na mzee," aliagiza.

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu huyo, Mkoa wa Arusha ndiyo kinara wa matukio ya ukatili ukiwa na matukio 4,320 ukifuatwa na Ilala matukio 2,680, Tanga matukio 2,257 na Kinondoni matukio 1,985.

Alibainisha kuwa kati ya Januari hadi Desemba mwaka jana, matukio 29,373 yaliripotiwa katika madawati ya jinsia, yakiongozwa na matukio 6,305 ya ubakaji nchi nzima.

Awali, Mwakilishi wa Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi Makao Makuu, Mary Kipesha alisema wameweka mkakati wa kutokomeza ukatili wa watoto kila mkoa, wilaya mpaka ngazi ya kaya, wakitoa elimu hadi shuleni.

"Ukatili ni sawa na wizi wa ng'ombe, hivyo tunauchukulia ni sawa na uhalifu mwingine. Familia tusimalizane kienyeji na tusilazimishe watoto kuolewa," Kipesha alionya.





## TADB yawekeza katika elimu watoto wa kike

**Na Anjela Mhando,** SIHA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imejitosa kung'arisha ndoto za kielimu za watoto wa kike wa jamii ya kifugaji ya Kimasai wanaopata elimu katika Shule ya Sekondari Esinyari, ikiahidi kuchangia mifuko 300 ya saruji kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bweni la wasichana.

Shule hiyo ni maalum kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaotoka kaya zenye jamii za kifugaji katika Kata ya Orkolili na Kata jirani ya Ormelili kufikia ndoto zao.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Orkolili alikokwenda kuzungumza na wakazi wa wilaya hiyo, Mkurugenzi wa Fedha wa TADB, Kanaeli Nnko alisema uamuzi huo unalenga kuhakikisha mtoto wa kike wa jamii hiyo ya kifugaji, anasoma na kutimiza ndoto zake za elimu bila kukatishwa na vikwazo vyovyote ikiwamo umbali wa kufika shuleni.

"Nikiwaona hivi ninyi watoto wa kike, nikiambiwa mnaenda kuolewa, ninaweza kulia kwa kuwa mimi nina watoto wadogo kama ninyi. Ninawaomba muendelee na elimu yenu. Elimu siyo kwenda tu kidato cha nne na kidato cha tano, kuna vyuo vya ufundi, vyuo vya ualimu, vyuo vya uuguzi na kadhalika.

"Benki ya Kilimo inategemea miaka minne ijayo iwaone wengine ni walimu na madaktari lakini pia wakurugenzi. Nimechagua kuchangia ujenzi wa bweni na ninaomba niseme nimekubaliana na ninyi kwamba kusoma shule ya kutwa kwa mtoto wa kike ni jambo gumu sana. "Katika kujitoa huko, mimi na familia yangu tupo tayari kuchangia mifuko 300 ya saruji kwa kuanzia, lakini pia sitaishia hapo, nitamwomba Mkuu wa Shule ashirikiane na Kamati ya Shule waniandalie fomu ambayo nitachangisha, nitaipitisha kwa marafiki zangu kwa ajili ya kusaidia ujenzi huo," aliahidi.

Mkuu wa Shule hiyo, Denis Kagusha wakati wa mahafali ya kwanza ya shule hiyo, alisema hawana bweni hata moja kwa ajili ya wanafunzi wa kike, suala ambalo limeleta ugumu katika utendaji na mahudhurio ya wanafunzi darasani.

"Tatizo hilo la kukosekana kwa mabweni limekuwa likisababisha wanafunzi wengi kupata ujauzito na kukatisha ndoto yao ya kimasomo. Pia, baadhi ya wazazi wa jamii ya kifugaji, wanawalazimisha watoto wao wa kike kuacha shule ili wakaolewe," alisema.

Diwani wa Orkolili (CCM), Jonathan Nassari alisema alilazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam kumfuata Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Kilimo ili kumwomba akubali kuwapiga jeki katika ujenzi huo wa bweni la wasichana.

# CHADEMA wajitosa sakata uvamizi wa chanzo cha maji

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SAKATA la chanzo cha maji cha Isanja kilichoko Kata ya Nasai wilayani Siha mkoani Kilimanjaro kudaiwa kuvamiwa na makundi ya mifugo kutoka wilaya jirani za Longido na Simanjiro na kuharibiwa kutokana na mwendelezo wa shughuli za binadamu, limekiibua Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Chanzo hicho cha maji kinazungukwa na vijiji sita, kikiwamo cha Koboko Kaskazini. Inaelezwa kuwa wafugaji kutoka wilaya jirani wamekigeuza chanzo hicho sehemu ya malisho ya mifugo. Katika taarifa yake kwa umma, Katibu wa Uenezi wa CHADEMA Wilaya ya Siha, Robert Mrisho, alisema jana kuwa chama hicho kinafuatilia uhalali wa kundi la mifugo, kuvamia maeneo ya Isanja, Kata ya Nasai.

"Chama kama taasisi inayotokana na wananchi, kinafuatilia taratibu za kisheria juu ya uhamishaji na usafirishaji wa makundi ya wanyama (mifugo) ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa milipuko ya magonjwa ya mifugo.

"Kwanini chama kinafuatilia jambo hili? Lengi ni kuepusha uharibifu kama ule uliotokea kule West Kilimanjaro, na hii ni kwa sababu tunaamini serikali ni moja na sheria ni zilezile.

"Kama chama, tunaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Siha kulifuatilia jambo hili kwa kuwa zizi linalotumika kuhifadhi makundi ya ng'ombe, mbuzi na kondoo, limejengwa kwa Mwenyekiti wa Kijiji," alidai.

Kutokana na uvamizi huo wa chanzo cha maji, Mrisho alisisitiza CHADEMA inasukumwa na taarifa kwamba eneo hilo tayari limeshachomwa moto na wanaona si dalili nzuri kwa ustawi wa usalama wa wananchi wa Nasai.

Siku chache zilizopita, Ofisa Tarafa ya Siha Kaskazini, Asteria Alfred alinukuliwa akisema kuwa kutokana na kujitokeza kwa madhara katika chanzo hicho, ameagiza viongozi wa serikali za vijiji na vitongoji kukilinda kwa hali na mali chanzo hicho dhidi ya wavamizi.

"Kuanzia Oktoba 11 mwaka huu, tumeanza kutumia sheria ndogo inayoelekeza kwamba yeyote atakayekutwa ameingiza mifugo kwenye chanzo hiki, faini ya kila mifugo ni Sh. 25,000, na ninyi wananchi wa Isanja, watangazieni kabisa na wengine, hasa hao wavamizi kwamba 'muziki ni mnene', hatutawachekea maana nia yao sio njema," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumia Maji ya Mto Sanya, Goodchance Moshi aliyekwenda kuzuru eneo hilo kujionea madhara hayo, alisema ni wajibu kwa viongozi hao kukilinda chanzo hicho ili maji yaendelee kuwapo kwa kizazi cha sasa na kinachokuja.

"Sheria Namba 11 ya Mwaka 2009, imefafanua wazi kwamba chemichem, matindiga na maeneo oevu kama hili la Isanja, yanatakiwa kulindwa kisheria na vijiji vinavyolizunguka eneo hilo bila kungoja serikali kuu.

"Mtu anapokuja na kuanza kulima au kuingiza mifugo, serikali ya kijiji inatakiwa kumchukulia hatua. Kwa sababu ndani ya mita 60 hakutakiwi kufanyika shughuli za kibinadamu," alisema.



Mratibu wa Mradi wa Shirika lisilo la kiserikali la Support For Future Foundation" (S4F) linalojishughulisha na kuwasaidia watoto na vijana wenye ulemavu Kanda ya Kaskazini, Zabibu Sindangu (kushoto) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa S4F, Dk. Sylvia Ruambo (kulia), wakimpandisha mtoto mlemavu, Hassan Hatibu Ally kwenye kiti cha magurudumu manne baada ya kumkabidhi kilichotolewa msaada na shirika hilo, katika Mtaa wa Michungwani, wilayani Muheza juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanafunzi wawagusa wapinga ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Sikirari iliyoko Kata ya Donyomoruwak, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wamewaliza baadhi ya wananchi na wanaharakati baada ya kukumbusha namna wanawake wanavyoumizwa na vitendo vya rushwa ya ngono ili kupata huduma katika jamii.

Baadhi ya wakazi wa Sikirari waliokuwa wakifuatilia maudhui hayo jana yaliyokuwa yanatolewa na wanafunzi hao kupitia Klabu ya Sauti Yangu, Nguvu Yangu, walijikuta wakinong'ona na kuzusha mjadala kuhusu vita dhidi ya ukatili wa kijinsia inavyoibua hamasa ya kukataa ukatili huo.

Akizungumzia hali ya ukatili katika jamii, mwanafunzi Michael Issaya alisema matukio yanayofifisha ustawi wa watoto wa kike kwa muda mrefu sasa ni ubakaji, kulazimishwa kuolewa, kunyimwa haki ya elimu, kuunguzwa na pasi sehemu mbalimbali za mwili, kukatwa viungo vya mwili na kukeketwa.

"Wanasikirari wenzangu, wana Kilimanjaro na Watanzania kwa ujumla, hakika wahenga hawakukosea kusema Mungu si Athumani, si Abdallah wala Juma. Mungu ni wa tofauti sana na viumbe vyote vilivyomo ulimwenguni.

"Ninayasema haya kwa sababu Mungu aliyahurumia yale makundi mawili, yaani wanawake na watoto yaliyofanyiwa ukatili wa kijinsia, hivyo alimtuma mtumishi wake Fredrick kuanzisha Shirika liitwalo KWIECO (Kilimanjaro Women Information Exchange Community Organization) inayohusika na masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia mkoani Kilimanjaro.

"Looh! ninasikitika sana eti mwanadamu anafanywa kama bidhaa sokoni, sisemi wazazi wasidai mahari pindi binti yao anapotaka kuolewa, La hashaa! Ila wazazi wasiwashurutishe binti zao kuolewa kwa kuwapigia debe kwa vijana kwamba binti zao ni wazuri kama jinsi bidhaa za sokoni zifanyiwavyo.

"KWIECO wamefanya makubwa katika kuhakikisha ukatili wa kijinsia unakoma mkoani kwetu, wamekuwa wafuatiliaji wazuri wa klabu shuleni. Vilevile, wamekuwa wadau wakubwa wa kutoa elimu kwa wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu ukatili wa kijinsia, kweli mmeupiga mwingi!" alisisitiza.

Mradi wa Jamii Salama kwa Maendeleo Yetu, Sauti Yangu, Nguvu Yangu, Tupinge Ukatili wa Kijinsia, unatekelezwa na KWIECO katika vijiji 12 kwa ufadhili wa Taasisi ya Kimataifa ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom (FNF).

Vijiji vinavyonufaika ni Donyomoruwa, Orkolili, Kilingi, Ngumbaru, Fuka, Koboko Kusini, Embukoi, Lekrumuni, Magadini, Namwai, Gararagua na Mlangoni.

Akizungumza na wananchi na wanafunzi hao, Mratibu wa Mradi huo, Elizabeth Mushi alisema vilio vya wanawake kuanzia huko nyuma hadi sasa, vingi viliishia mikononi mwa mila na desturi potofu.

Alisema mila hizo zilizowakandamiza na kuwatumia wanawake kama nyenzo ya kupata mali katika jamii, pia zilitumika kuwashurutisha kuolewa ili wazazi wapate mahari kwa ajili ya kuendesha maisha yao.



## HABARI DODOMA

## Wazazi walalamika jiko ndani ya darasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZAZI wa watoto wenye mahitaji maalum wanaosoma katika Shule ya Msingi Mlezi jijini Dodoma, wamelalamikia kuwapo kwa karo la maji na jiko ndani ya darasa wanalolitumia watoto wao.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo kwa wazazi wanaoishi na watoto wenye mahitaji maalum yaliyoratibiwa na Taasisi ya Special Olympics, mmoja wa wazazi hao, Evodius Wilfred alisema hali hiyo ni hatari kwa watoto wao.

Alisema kuwa kutokana na shida za kimaumbile walizonazo watoto wao, baadhi wakiwa na ulemavu wa akili, kuwa na karo la maji na jiko ndani ya darasa hilo ni hatari.

"Darasa lile lina watoto kama 80 hivi lakini pia limezungushwa uzio ambao unawanyima haki ya kucheza watoto mbali na kuwapo karo la maji pamoja na jiko"alisema.

Mzazi huyo alisema wamekuwa wakiulalamikia uongozi wa kata kupitia kwa diwani wao lakini hakuna jitihada ambazo zimefanyika hadi sasa kunusuru hali hiyo.

"Kila siku tunaambiwa fedha zitatoka kwa ajili ya kujenga madarasa ya kutosha kwa watoto lakini hakuna kilichofanyika hadi sasa na watoto bado wanaendelea kusoma katika darasa hilo moja," alisema.

Akizungumzia suala hilo, Ofisa Elimu Maalum wa Jiji la Dodoma, Issah Kambi alikiri shule hiyo ina shida ya miundombinu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum na jitihada zinafanyika ili kukabili hali hiyo.

"Tayari Jiji limeshatenga Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo ujenzi wa mabweni kwa ajili ya watoto hawa wenye mahitaji maalum," alisema Kambi.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu Maalum Shule ya Msingi Mlezi, Hashim Msemo alisema uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalum katika shule hiyo ni mkubwa kulinganisha na idadi ya walimu waliopo.

"Uandikishaji watoto katika shule hii ni mkubwa sana kuliko idadi ya walimu waliopo na hawa watoto wenye tatizo ulemavu wa akili pamoja na usomaji, wana shida sana na ni wasumbufu sana, hivyo kuweka uzio ni moja ya kuwalinda kutokana na mazingira yetu.

"Pale shuleni kuna barabara ambayo inatumika na magari mengi, hivyo bila uzio ingekuwa shida kuwadhibiti lakini hilo karo linalolalamikiwa ni lile ambalo lilikuwapo wakati wa ujenzi wa madarasa na lile jiko pale lilipo hakuna shida sana kwa watoto hawa," alisisitiza Msemo.

# TARI kumaliza uhaba mbegu za muhogo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kutekeleza mpango mkakati wa miaka 10 unaolenga kuongeza uzalishaji wa zao la muhogo kufikia tani milioni 24 ifikapo mwaka 2030, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeingia makubaliano na kampuni za mbegu ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa mbegu.

Akizungumza jana kwenye hafla hiyo jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo.

Alisema kwa sasa Tanzania inazalisha tani milioni 8.2 za muhogo na kwamba makubaliano hayo yataongeza uzalishaji wake.

"Taasisi ya MEDA imekuwa kiunganishi kwetu kuhakikisha suala la mbegu kwenye zao la muhogo linachukua nafasi kubwa, suala la mbegu tumepanga kuweka mfumo ambao ni endelevu, kampuni zitazalisha mbegu za daraja la juu,"alisema.

Alibainisha kuwa lazima kuweka nguvu kubwa kwenye uzalishaji wa mbegu bora ambazo zimeidhinishwa na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na makubaliano hayo kwa sasa wameingia na kampuni sita ili kuzalisha mbegu kwenye madaraja ya msingi.

"Kutokana na umuhimu wa sekta binafsi kama kampuni inaonyesha nia ya kuzalisha mbegu ya aina fulani ambayo ni kipaumbele kwetu, kuna utaratibu sasa hata wa kuwapa ardhi ili kuzalisha mbegu," alisema.

Alisisitiza kampuni zilizopata fursa hiyo kuwa wazi kama hazina ardhi ili zipatiwe na zizalishe mbegu.

Meneja Mradi wa Muhogo kutoka Taasisi ya MEDA, Stephen Magige alisema zao hilo lina uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambapo uzalishaji wake ulikuwa unapungua hadi tani 5.5 kwa ekari, sababu kubwa ikiwa ni magonjwa ya batobato ambayo hupunguza uzalishaji kwa asilimia 80.

"Kwa sasa kuna mradi wa Best Cassava upo awamu ya pili ukilenga kuwa na mfumo endelevu wa upatikanaji wa mbegu bora za muhogo. Kupitia miradi miwili ya muhogo tumekuwa na aina 10 za mbegu ambazo zina uwezo wa kuhimili magonjwa," alisema. Aliongeza kuwa kwa sasa kuna wakulima wajasiriamali 700 ambao wanazalisha na kuuza mbegu.

Awali Mwenyekiti wa Chama cha Wazalishaji na Wasindikaji wa Muhogo (TACCAPA), Mwantumu Mahiza alisema watu wengi wamehamasika kulima muhogo na lilipatikana soko kubwa linalohitaji tani milioni mbili za muhogo mkavu hadi sasa halijafanikiwa.

"Hii ni changamoto kubwa kwa serikali yetu kwa sababu mazao makubwa tunalalamika hayana soko, lakini soko linavyokuja linakuja na vigezo vyake wengi tunashindwa kufikia," alisema.

Aliongeza kuwa vijana wengi wamehitimu vyuoni lakini hawana ajira, akisisitiza kuwa zao hilo ni mkombozi kwao kama wakipatiwa maarifa na mitaji.

"Tumejiandaaje kuhakikisha kilimo kinapendwa na vijana maana picha tunazotumia ni za wakulima waliochoka, hajavaa vizuri, tunatakiwa tupige picha zinazoonyesha matumaini ili vijana wavutiwe," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wazalishaji wa Mbegu Bora za Muhogo Kanda ya Mashariki, Burton Nsape alishukuru kwa makubaliano hayo yatakayosaidia kusogeza huduma kwa wakulima.




Mmoja wa maofisa wa Jiji la Dodoma, Onesmo Mlongwa (katikati), akitoa elimu ya namna ya kunawa mikono jijini humo jana, ili kujikinga na magonjwa ya kuambukiza, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho yanayoendelea ya wiki ya kunawa mikono Duniani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC ataka bajeti kukabili vifo vya mama na mtoto

**Na Renatha Msungu,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda ameitaka Halmashauri ya Wilaya hiyo kutenga bajeti kwa ajili ya kuendeleza mradi wa afya ya mama na mtoto unaotekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania ili kuendelea kupunguza vifo kwa makundi hayo.

Mradi huo umefadhiliwa na Serikali ya Ireland na umetekelezwa kwa muda wa miaka mitano katika wilaya za Bahi na Chemba chini ya usimamizi wa shirika na serikali.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa mradi huo kwa halmashauri hiyo, Mwanahamisi alishukuru wafadhili Ireland na World Vision kutokana na kusaidia kuepusha vifo vya mama na mtoto.

"Nimesikia maelezo ya watoa huduma za afya ngazi ya jamii walivyoeleza ugumu uliokuwapo wakati wa kutoa elimu kwa jamii ya kuhudhuria kliniki kwa mjamzito na mtoto, hivyo elimu tumeshapewa, wafadhili wanaondoka, nasi tuiendeleze ili tuzidi kuwa bora," aliagiza.

Mkurugenzi wa Shirika la World Vision Tanzania, Gilbert Kamanga alisema jamii imepata uelewa ambao utatumika kuendeleza mradi huo.

Alisema kuwa katika vijiji 13 ndani ya Wilaya ya Bahi ambavyo mradi huo umetekelezwa, kuna mabadiliko makubwa hususan kwa wajawazito kuanza mapema kuhudhuria kliniki, tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya elimu hiyo kutolewa kwa jamii.

"Ninaishukuru sana serikali kwa ushirikiano iliotoa wakati wa utekelezaji wa mradi huu, ninaamini halmashauri itaendeleza yale yaliyofanywa na wafadhili chini ya usimamizi wa World Vision Tanzania," alisema Kamanga.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Maira Biseko alisema mradi huo umechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya mama na mtoto tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema kwa mwaka huu hakuna vifo vilivyotokea kutokana na uzazi, ikiwa ni matokeo chanya ya mradi huo, wajawazito sasa wanaanza kliniki mapema pindi wanapopata ujauzito.

Meneja wa Programu Ubalozi wa Ireland nchini, Katarina Mungure alisema wametumia Sh. bilion 32 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.





# SMZ yakiri tatizo usafiri wa wagonjwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Fatma Mrisho, amesema bado kuna tatizo la usafiri kwenye vituo vya afya katika kuokoa maisha ya wajawazito na watoto wachanga wanapokuwa na dharura za kiafya.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar wakati akizindua mpango wa uimarishaji huduma za 'M-Mama' za rufani na usafirishaji wa dharura kwa wajawazito, walioijifungua na watoto wachanga.

Katibu mkuu huyo alisema changamoto hiyo itatatuliwa na mfumo huo wa usafiri wa dharura ambao umehakikiwa katika mikoa ya majaribio ikiwamo Zanzibar.

Alisema serikali itaendelea kutekeleza wajibu wake katika kuwafikishia wananchi huduma muhimu za afya kwa ajili ya maendeleo yao na taifa na tayari wizara imeweka huduma za mama na mtoto kuwa vipaumbele.

Kwa mujibu wa Dk. Mrisho, Wizara inathamini jitihada za wadau tofauti wa maendeleo katika kusaidia nguvu za serikali kutatua changamoto za afya, hasa kwa kuanzisha mfumo huo wa M-Mama ambao mafanikio yake yameshaonekana katika mikoa ya Tanzania Bara. "Wizara inaelewa kwamba moja ya masuala ya kuyafanyia kazi ni rufani kati ya vituo vya kutolea huduma za afya, hasa upatikanaji wa usafiri wa dharura kutoka kituo kimoja hadi kingine kinachoweza kutoa huduma ya viwango vya juu,"alisema.

Pia alisema kwa sasa Zanzibar ina magari machache ya kubebea wagonjwa ambayo hayakidhi mahitaji.

Naye Mkuu wa Idara ya TEHAMA katika Wizara ya Afya, Mohammed Habib Ali, alisema mradi huo una lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kuondoa ucheweleshaji wa huduma.

Alisema vifo hivyo vinatokana na kuchelewa kupata huduma kwa mama wajawazito ambapo uchelewaji wa aina tatu unahusishwa, ikiwamo mama kuchelewa kufanya uamuzi wa kwenda hospitalini, kuchelewa kupata usafiri na kuchelewa kupata huduma wakati muafaka.

Radhia Mataka, Ofisa Uzazi wa Mpango kutoka Kitengo Shirikishi cha Afya ya Uzazi na Mtoto, alisema afya ya uzazi na vifo vya mama na watoto bado hairizishi. Alisema takwimu kutoka Hospitali ya Mnazi mmoja, Julai hadi Septemba, mwaka huu, zinaonyesha kinamama 10 wamefariki dunia kwa uzazi Zanzibar.

"Hizi ni takwimu za hospitali tu hatuna takwimu zilizotokea katika jamii kiufupi hali hairidhishi" alisema

Alisema vifo vya wajawazito vinatokana na wengi wao kuchelewa kupata huduma mapema na hufika hospitalini wakiwa katika hali mbaya ya kiafya.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kinamama wengi wanasubiri mpaka mimba ikue miezi sita ndipo waende kliniki wakati huwa tayari matatizo yameshajitokeza na kuchelewa kupata huduma ya afya ya uzazi wakati wanatakiwa wahudhurie kliniki mimba inapoanza.

Alisema tatizo lingine linalosababisha vifo ni upungufu wa damu mwilini kwa wajawazito wakati damu inahitajika mwilini ili kufanya afya ya mama na makuzi ya mtoto kuwa mazuri.

Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Simu ya Vodacom, Alex Bitekeyo, alisema wametenga dola milioni 1.5 kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mradi huo ambao kwa upande wao watasaidia huduma za mawasiliano kwa kinamama wanaohitaji huduma za kujifungua.

## Mwinyi ataka watanzania ughaibuni kuwekeza nchini kukuza maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amekutana na Watanzania wanaoishi na kufanya kazi Oman katika ziara yake nchini humo yanye lengo la kuimarisha uhusiano mzuri uliopo kati ya Oman na Tanzania na kutafuta fursa za biashara zitakazojenga uchumi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana katika ziara yake hiyo ya kikazi nchini humo na kusema kuwa ni wakati mwafaka wa kuwekeza Zanzibar kwa sababu hali ya amani na utulivu imeimarika.

Dk. Mwinyi alielezea sera ya uchumi wa bluu na kuainisha mambo matano inavyojikita serikali yake katika kuingia katika sera hiyo.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni utalii, uimarishaji bandari kubwa eneo la Mangapwani, uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na usafiri wa bahari.

Rais Dk. Mwinyi alisema ili mambo yote hayo yaende vizuri ni lazima kuwe na nishati ya umeme wa uhakika, maji safi na salama, miundombinu bora ya barabara na mfumo mzuri wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Oman, Abdallah Abbas Kilima, alisema wanadiaspora wanaoishi Oman wamefurahia ziara yake hiyo ya siku nne iliyoanza Oktoba 10, mwaka huu.

Akisoma taarifa maalumu ya wana diaspora, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanadiaspora wanaoishi Oman, Suleiman Yussuf, alisema wamempongeza Rais Mwinyi na viongozi wengine wa vyama vya siasa Zanzibar na Tanzania kwa kuondoa tofauti za muda mrefu na kutengeneza Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo hadi sasa ina mwelekeo mzuri wa masikilizano .



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk Mzuri Issa (kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UNWOMEN), Sima Sami Bahous aliyetembelea katika ofisi za TAMWA Tunguu Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wapongeza mradi wa kuwezesha wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), Zanzibar Dk. Mzuri Issa, amesema mradi wa kuwawezesha wanawake katika uongozi, maarufu kama Wanawake Wanaweza, umesaidia kuwajengea uwezo wanawake wa Zanzibar katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha pamoja kati ya TAMWA, uongozi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kutetea Haki za Wanawake (UN Women), uliongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, ambae pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Sima Sami Bahous.

Katika mkutano huo uliofanyika Ofisi za TAMWA, Tunguu, Zanzibar, Dk. Mzuri alisema bado wanawake na vijana wanakabiliwa na vikwazo vingi katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo rasilimali fedha na rushwa.

Kutokana na vikwazo hivyo, alisema nguvu za pamoja zinahitajika katika kuondosha mikwamo inayowakabili pamoja na kuendelea kuwajengea uwezo.

Alipongeza juhudi za mashirika ya maendeleo, likiwamo UN Women katika kuwashajihisha wanawake kufikia malengo ya usawa wa kijinsia na kuwania nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali ikiwemo katika vyombo vya kutunga sheria.

Wakitoa ushuhuda wa mafanikio ya mradi huo mbele ya ugeni huo, wanawake wanasiasa walisema umekuwa mkombozi kwao kwa sababu umefungua milango ya kuaminiwa katika jamii kuwa viongozi.

Halima Ibrahim kutoka chama cha ACT WAZALENDO, alisema mradi huo umewajengea uelewa wa kujitambua kuwa wanawake wanahaki, katika uongozi na kuondokana na mawazo mgando kuwa mwanamke ni mama wa nyumbani.

"Tunaipongeza sana TAMWA kwa kutuweka pamoja wanawake kutoka vyama tofauti vya siasa na kutupatia elimu kuhusu uongozi kwa mwanamke. Elimu hiyo imezaa matunda kwa sababu wanawake wengi walijitokeza kugombea nafasi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020" alisema.

Pia alisema mradi huo iliokuwa ukiendeshwa na TAMWA pia umewasaidia kujiamini na kuthubutu kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa ndani ya vyama ambapo kwa miaka mingi wanawake waliachwa nyuma katika nafasi hizo.

Aliwataka wanasiasa wanapokua katika majukwaa ya kisiasa kushindana kwa hoja na si kutunishiana misuli ili wanawake kutokuwa woga kugombea nafasi za uongozi.

Mkurugenzi Mkuu wa UN Women, Sima Sami Bahous, alisema wataendelea na juhudi za kuwajengea uwezo makundi mbalimbali ya wanawake kugombea nafasi za uongozi ili kuingia katika vyombo vya kutunga sheria.

Alisema sauti za wanawake zinaweza kufikiwa kama watashiriki kugombea katika nafasi za kuchaguliwa hatua ambayo itawafanya kuingia katika vyombo vya maamuzi na kutunga sheria.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



**LALA SALAMA RICO SWAVEY**
Soma Uk.14

JUMAMOSI OKTOBA 15, 2022



# NI YALE YALE

## Yaliyomliza Harmonize, Chiddy yamtoa kamasi

Ukurasa.15



# SALUM ABDALLAH-1



## • Mtoto mboga saba wa kiarabu
## • Mtunzi wa kibao pendwa Mkono wa Iddi

**Na Adam Fungamwango**

"Minal Faidhina, mpenzi wangu Minal Faidhina, kwa mapenzi na furaha, mpenzi wangu mi nakupa, mkono wa Idd."

Huu wimbo maarufu sana ambao husikika kila mwaka wakati wa sikukuu ya Idd El Fitri. Ni wimbo wa miaka na miaka na vizazi vingi vimeukuta na kuufurahia.

Pamoja na kuufahamu wimbo huo, lakini wengi wao hawajui umepigwa na bendi gani na hata kumfahamu mwimbaji na mtunzi wa wimbo huo.

Moja kati ya matukio ambayo wakazi wa Morogoro, mashabiki wa muziki Tanzania na Afrika Mashariki hawatoyasahau ni kuondokewa na mwanamuziki bora nchini, Salum Abdallah Yazidu (SAY), na kuacha majonzi makubwa.

Ilikuwa Novemba 18, 1965 alipofariki mwanamuziki huyo ambaye tayari alishakuwa maarufu ukanda wa Afrika Mashariki.

Alifariki dunia baada ya kupata ajali ya gari, pale tairi lilipochomoka kwenye lori la mchanga alilokuwa akiendesha.

Baadhi ya nyimbo zake zilizompatia umaarufu mkubwa ni 'Ngoma Iko Huku', 'Shemeji Shemeji','Mkono wa Idd', 'Wanawake Tanzania', 'Sipati Majibu,' 'Naumia', 'Cuba Chacha' na 'Ewe Mola Wangu', ambao wachambuzi wengi wa masuala ya muziki wanadai kuwa ni kama alikuwa akitabiri kifo chake.'

Ni mmoja wa wanamuziki wa kizazi cha kwanza cha muziki wa Tanzania, ambaye ndiyo msingi wa wanamuziki wengi waliofuatia nchini akiwamo marehemu Mbaraka Mwinshehe Mwaruka ambaye naye ni zao la Salum akitokea huko huko mkoani Morogoro.

**Alikuwa mtoto wa mboga saba**

Mara nyingi wanamuziki wengi hutoka kwenye familia za kimasikini, lakini haikuwa kwa Salum Abdallah. Yeye alitoka kwenye familia ya kitajiri. Baba yake mzee Abdallah Yazid alikuwa Mwarabu aliyetokea nchini Yemen na kuja nchini kutafuta maisha na kujikita mkoani Morogoro,, aliyemuoa binti mmoja Mtanzania mkazi wa Morogoro.

Alikuwa ni mfanyabiashara mkubwa akimiliki migahawa kadhaa Morogoro mjini, maduka na magari madogo na makubwa.

Salum aliyezaliwa Mei 5, 1928, alilelewa kwenye mazingira hayo ya kitajiri, watoto wa mjini kwa sasa wanayaita 'mboga saba', lakini tayari kwenye kichwa chake kulikuwa na wito wa muziki.

Akiwa mdogo, alikuwa anapenda kwenda kwenye nyumba za jirani ambazo zilikuwa na mashine za santuli, maarufu kama 'rekodi pleya', na wakati huo nyimbo zilizokuwa zikivuma ni za zile za kutoka nchini Cuba, kama vile macharanga, salsa, borelo, ambazo zilikuwa kwenye santuli zilizoitwa GV.

Baba yake alimuweka kwenye moja kati ya maduka yake, lakini mara kwa mara alikuwa anatoroka na kwenda kusikiliza nyimbo hizo, kitu ambacho kilikuwa kinamkasirisha sana baba yake na kumcharaza bakora mara kwa mara.

Mtoto hakukoma, kiasi kwamba baba akaamua kubadilisha mbinu, akaamua kumnunulia 'pleya' ili kijana wake atulie dukani.

Hiyo ndiyo ilikuwa dawa, kwani Salum sasa alitulia dukani na kufanya biashara vizuri kiasi baba yake alifurahi na kuzidi kumpenda, licha ya kwamba alikuwa hapendi kuona kijana wake akipenda sana muziki, hasa huu wa dansi ambao yeye itikadi yake haikukubaliana nao.

Alipoanza kupata makamo, akiwa na miaka 15 hadi 17 hivi, baba yake alikuwa akimtuma jijini Dar es Salaam kununua bidhaa kwa ajili ya maduka yake.

Hii ilimpa sana nafasi na uhuru Salum kujiingiza zaidi kwenye muziki kwani wakati tayari ameshafungasha mizigo yake kurejea Morogoro akiwa jijini Dar es salaam kujimwaga kwenye kumbi za starehe, hasa bendi yake kubwa aliyoipenda ni Dar Jazz.

**Itaendelea wiki ijayo**

# NI YALE YALE

## Yaliyomliza Harmonize, Chiddy yamtoa kamasi



MGOGORO ulioibuka kati ya mwanamuziki maarufu Harmonize, na wasanii wake wawili Killy na Cheed, umeibua hisia tofauti, huku baadhi wanasema ni mwendelezo wa mambo yanayoutafuna muziki wa Bongo Fleva.

Hivi karibuni Harmonize na uongozi wake wa Konde Music Worldwide umetangaza kuachana na wasanii hao na kuwataka wawe huru kufanya kazi nje. Hata hivyo, Killy na Cheed wamekimbilia kufika Baraza la Sanaa (Basata) kuomba msaada ili kujua sababu ya wao kukatishwa mkataba.

Kinachosikitisha Harmonize na uongozi wa lebo hiyo, juzi walipotakiwa kufika ofisi za Basata, Kivukoni Dar es Salaam, hawakufika jambo linalooneka-na kuleta ukakasi.

Hata hivyo, chanzo kimoja kilieleza Harmonize na wenzake walishindwa kufika kikaoni kutokana na kukosa nafasi kwa kuwa walisafari kwenda nchini Afrika Kusini kwa ajili ya ku 'shoot' video na kuahidi kwamba wangeweza kufika kikaoni kuanzia Novemba 18, jambo ambalo Basata hawajakubaliana nalo na kutoa amri ya kufika kikaoni wiki ijayo.

Baadhi ya wachambuzi wa muziki, wamesema anachokifanya Harmonize anarudia yaleyale aliyokuwa akilalamikia alipokuwa lebo ya Wasafi.

Abdul Mkeyenge, amesema muziki wa Bongo Fleva umetawaliwa na visasi, chuki na wivu na kusababisha kila unapotaka kwenda mbele unarudi nyuma.

"Harmonize kipindi kile alikuwa akilia alipokuwa Wasafi, alipoondoka tulitarajia yeye angekuwa mtu wa mfano kuweka sawa, lakini anarudia yaleyale aliyokuwa akiyakataa," amesema Mkeyenge.

Amesema, wasanii waliovunjiwa mikataba yao wana haki ya kutaka kujua, ni vyema Harmonize na timu yake ingefanya uungwana kwa kwenda Basata, kuliko kutokwenda kabisa.

"Hakuna anayejua sababu ya wao kufukuzwa, lakini harmonize angekumbuka yale aliyokuwa akilia zamani na yeye kuwa mtu wa mfano kuendelea na misuguano ni alama ya watu kushindwa kubadilika na kubaki na misimamo ya zamani," ameongeza kusema.

Kwa upande wa Meneja wa wasanii hao aliyejitambulisha kwa jina la Sats Sembe, amesema sababu ya wao kufikisha malalamiko yao Basata ni kupinga utaratibu wa kuvunja mkataba na wasanii hao ambapo alieleza kuwa hakuna barua yoyote ya maandishi waliyopewa.

"Huko mbeleni hatujui hili suala litafika hapa, lakini kwa kuanzia tumeanzia kwa walezi wetu na wazazi wetu Basata ambao katika hali ya kawaida tusingeweza kuwaruka" amesema Sembe.

Sembe, ameonya endapo ikishindikana wataenda mahakamani kudai haki yao,

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**masanjamkandamizaji**
Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu; Nitatumaini wala sitaogopa; Maana Bwana YEHOVA ni nguvu zangu na wimbo wangu; Naye amekuwa wokovu wangu



**ireneuwoya8**
Yani leo ndio nimejua zile hesabu za kipeuo cha pili na kutafuta x ... ndio Haya maisha tunaishi



**wemasepetu**
Kama bado mna makasiriko nawaonea huruma... Tukubali yaishe jamani.. Mengine tunamuachia Mungu.



**auntyezekiel**
Leo tuna upande wa kina baba jamani je kina baba ushawahi kuzaa na mtu hadi ukajuta!!!sio kwa vibaya ila ukasema nilikitafita nini mie!!

BASI SAWA

## Kise apata mapacha

MWIGIZAJI na mwongozaji wa filamu nchini, Festo Kise na mkewe hatimaye wamepata watoto watoto wawili mapacha.

Akizungumza na BT, Kise, amesema huo ni uzao wake wa kwanza na anachoshukuru Mungu watoto na mama yao wana afya njema na ujio wao utamuongezea juhudi ya kufanya kazi zaidi.

"Imekuwa baraka kwenye familia yangu, mimi na mke wangu kupata watoto mapacha ambao ni Jayda na Jarden, hili ni jambo la furaha kwetu tumeona ni vizuri na mashabiki zetu wakajua," amesema Kise.



## PrayGod Sawe aridhika mafanikio



MWANAMUZIKI wa Injili PrayGod Sawe, amesema wimbo wake unaotamba 'Nimeridhika', umemfikisha katika kilele cha mafanikio kutokana na kumuunganisha na watu wengi wenye mamlaka.

Akizungumza na BT, Sawe amesema ngoma hiyo aliyomshirikisha Godfrey Steven, imemtimizia ndoto ambayo ilikuwa ikimtesa ya kumfanya kuwa mnyenyekevu zaidi kwa Mungu na kuwa karibu na viongozi mbalimbali.

"Yaani mtu bila Mungu anakuwa mkiwa, ni kama yupo jangwani tu, hata upate vitu vyote lakini mwisho wa siku havitakusaidia kitu, Ile Mungu kuniinua na kuonyesha mbele ya mamlaka inatosha kwangu kuita mafanikio kwangu," amesema Sawe.




## Genevieve ukweli mchungu

MISS Tanzania 2010 Genevieve, amejikuta akimkabili mwanamuziki nyota nchini, Nandy akimwambia kama hakuna ukweli na uhalisia hawezi kupata mafanikio.

Kauli hiyo ameitoa wakati akijibu ujumbe wa nandy ambaye amesema sasa ni muda wa wasanii wa kike kuwa juu kimuziki..

"Maneno yake ni mazuri lakini yanatakiwa yawe ya ukweli maana kuongea ni rahisi, vitu vinatakiwa viwe kiuhalisia kuanzia kusapotiana kwa wasanii wa kike kwa sababu hilo halipo" amesema Genevieve.



## Mpigieni kura Zuchu

MWEZI unaokuja Tanzania itaonyesha nguvu zake katika muziki, pale msanii anayetamba kwa sasa Zuchu atakapopambana na wanamuziki wakongwe wa Afrika kuwania tuzo za MFV EMA.

Zoezi la upigaji kura limeanza wiki hii, kuwapa nafasi mashabiki wa muziki kumchagua msanii ambaye ataichukua tuzo hiyo ambayo ina heshima kubwa duniani.

Zuchu ni mwanamuziki pekee wa Afrika Mshariki ambaye amewekwa katika kipengele cha Mwanamuziki Bora wa Mwaka, akiwa anashindana na wasanii wengine wanne ambao ni Burna Boy (Nigeria), Tems (Nigeria), Ayra Starr (Nigeria), BlackSherif (Ghana) na Musa Keys (Afrika Kusini).

## Mapigo ma 5 Sikinde

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Oktoba umeingia na mambo yake kwani umekua mzuri kwa wale wasanii ambao hawana majina makubwa sana kwenye muziki wa bongo fleva.

Pamoja na kwamba hawana majina makubwa kihivyo kama wasanii wengine tunaowafahamu, lakini wameanza kuushambulia mwezi huu kwa kutoa ngoma kali ambazo zimeanza kuwa gumzo. Wakati wale mastaa wakiwa bado wanajipanga kutoa ngoma mwezi huu, baadhi ya wasanii wameonekana kuja juu na kuusaka ustaa kwa nguvu zote baada ya kuamua kufanya kweli.

Ni msanii wa kike staa Zuchu, yeye hajapoa, amemua kwenda nao sambamba na kuamua kutoa ngoma yake.

Inawezekana mpaka mwisho wa mwezi huu mastaa nao wakawa wamaeshaingia vitani, lakini kwa sasa majamaa wanaosaka ustaa wamekuja juu kisawasawa.

Hebu tuangalie ni wasanii gani ambao mwezo Oktoba wameamua kufanya kweli.

**Vany K-Nafurahi**

Msanii aitwaye Vany K yeye Oktoba Mosi tu akaamua kutoa ngoma yake aliyoiita 'Nafurahi'.

Ni ngoma ambayo imeanza kuvuta hisia za mashabiki wengi wa muziki wa bongo fleva kutokana na maneno na mapigo yaliyo kwenye pini hiyo.

**Moje Music-Till i Die**

Huyu ni msanii ambaye ameshatoa ngoma kadhaa kama 'My Woman', 'Wireless', 'I don't Forget' na nyinginezo.

Oktoba 2 ameshusha mzigo mwingine uitwao 'Till i Die' ambao umeshaanza kukonga nyoyo za mashabiki wa muziki huo. Ni msanii ambaye ameshaanza kujitengeneza njia kuelekea kwenye 'ustaa.'

**Darkid-Anirudie**

Ngoma hii 'Anirudie' imefyatuliwa Oktoba 3 na tayari taratibu imeshaanza kupenya kwenye masikio ya mashabiki wa muziki wa bongo fleva.

Darkid, msanii mwenye ngoma nyingi sana kama 'Habibi', 'My Wangu', 'Tunapendana', Nilie na Nani', 'Naanzaje' na nyinginezo. Hii sasa inaitwa 'Anirudie', ikitoka Oktoba 3. Ni wimbo wa masikitiko wa mapenzi, jamaa akilalamika kuachana na mpenzi huku akiwa bado anampenda. Bibie amechukuliwa na mwanaume mwingine, jamaa sasa povu linamtoka.

Katika kulialia anamwambia mpenzi wake wa zamani kuwa namba yake ni ile ile hajabadilisha, hivyo siku akitaka ampigie tu hakuna tatizo kwa sababu bado anampenda, ingawa anaheshimu maamuzi yake na ataendelea kumpenda na anajipa moyo kwa kusema mwisho wa siku wanaweza kurudiana.

**Zuchu-Kwikwi**


Staa pekee aliyetamba kwenye mwezi Oktoba mpaka sasa ni Zuchu akiwa ametoa ngoma yake akiita 'Kwikwi'.

Ngoma ilitoka Oktoba 4 na kabla ya leo hii, tayari ilikuwa imeshatazamwa na mashabiki zaidi ya milioni mbili.

Watu 2,099,254 walikuwa wameitazama pini hiyo kwa siku hizi chache ambapo wachambuzi wa masuala ya muziki wanasema inaweza kuvunja rekodi ya ngoma zake mwenyewe hali ikiendelea hivi hadi kumalizika kwa mwezi huu.

**Kiziwanda-Vibaya**

Kuna msanii anaitwa Kiziwanda, huku ametupia ngoma mmoja anayoiita 'Vibaya' ambayo nayo imeanza kufanya vyema kwenye redio na mitandao na kijamii kwa kuwa na watazamaji kibao.






## DODOMA; Mapenzi yanayopishana na wakati

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA nzima inajua kuwa Dodoma ni mji mkuu wa Tanzania, ila swali linakuja kwa nini filamu hii ambayo imewashirikisha wasanii kutoka nchi mbalimbali na kuigiziwa kwenye kisiwa cha mafya kwa nini inaitwa Dodoma.

Dodoma ni filamu ambayo inahusiana na wapenzi wanaopishana kwa wakati ili kuwa pamoja. Filamu inaanzia kwenye jiji la Dar es salaam ambako tunakutana na msichana anayeitwa 'Dodoma', ambaye Helen Hartman, amevaa uhalisia huo. Kiasili Dodoma ni mzaliwa wa kisiwa cha Mafia ambako ndiko bibi na babu yake wake wanapoishi. Babu wa Helen ni Mzee Chiro (Ahmed Olotu).

Akiwa anaishi katika jiji maarufu la Tanzania Dodoma anakutana na mfanyabiashara maarufu ambaye wanakuwa naye kimapenzi kijana huyo anajulikani kwa jina la Max nafasi hii imeigizwa na John Dumelo kutoka Ghana. Dodoma pindi apatapo nafasi ya kurudi Mafia hakosi kwenda kwa kuungana na familia yake pamoja na mpenzi wake wa utotoni. Anayejulikana kwa jina la Malick ambaye nafasi yake imechezwa na Van Vicka muigizaji kutoka Ghana.

Ingawa Dodoma na mpenzi wake wa utoto wanapendana inakuwa vigumu wao kuwa pamoja kutokana na pindi mmoja wao anapokuwa hana mpenzi mwingine anakuwa na mpenzi. Wanachukua uamuzi wa kupendana kwa mbali na kufurahia furaha ya kila mmoja wao.

Max mfanyabiashara maarufu sio mkweli katika pendo lake na Dodoma anakuwa na mpenzi mwingine na kusababisha kuachana na Dodoma. Wakati Dodoma akiwa tayari kumtaarifu kuwa hana mpenzi, Malick anamuwahi kwa taarifa njema kwake kuwa yuko tayari kumwoa mchumba wake Dk. Sherry ambaye nafasi hii imechezwa na muigizaji mchekeshaji kutoka Afrika Kusini Morike.

Filamu hii ambayo ina drama pamoja na vichekesho imeandikwa na kuongozwa na Honeymoon Aljabri. Ambaye alisema ameamua kuita filamu Dodoma ni kwa ajili ya kutaka kuutangaza mkoa ambao amekulia.

"Ukiangalia wenzetu wa nchi mbalimbali wanatabia ya kuita watoto wao majina ya miji, kuna Wengi waitwao Houston, London , Paris , Cairo na kuendelea. Mimi nimeamua kuita Dodoma ili kuupa nuru jiji ambalo nalipenda kuliko miji yote duniani"

Aliongeza kwa kuwa Dodoma ni makao makuu ya nchi, na huyu binti aitwaye Dodoma ndio mhusika mkuu ya filamu hiyo.

Honeymoon amesema kuwa ameamua kutumia kisiwa cha Mafia , kwa kuwa ni kisiwa chenye mvuto na madhari yake ni ya kipekee, hivyo hii pia itakitangaza kwa watu mbalimbali duniani.

Filam hii imetayarishwa na Eunice Karanja na ni filamu yake ya kwanza kuandaa na kueleza imekuwa na changamoto katika kutengeneza filamu bila kuwa na wafadhili.



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368



TWANGA

**Mjengoni Classic Band**
Bendi hii yenye maskani yake jijini Arusha, kwa sasa iko Dar es Salaam kwa muda, ambapo leo Jumamosi itatoa burudani katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, kesho itakuwa Kisuma Pub Temeke.

**HQ Band**
Kundi hili linaloongozwa na mwimbaji Rama Pentagon, leo Jumamosi litatoa burudani ndani ya ukumbi wa Kilimanjaro Pub uliopo Kiwalani, kesho litapumzika likijipanga kwa ajili ya wikiendi ijayo.

**Tukuyu Sound Band**
Wao Ijumaa na leo wapo jijini Arusha ambapo jana walikuwa ndani ya ukumbi wa Kipong na leo watakuwa na shoo maalum, kesho wataibukia jijini Dar es Salaam katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park.

**Msondo Ngoma**
Jana Ijumaa walikuwa katika onyesho maalum ndani ya ukumbi wa Diamond Jubilee, leo Jumamosi wapo ndani ya KB Tabata na kesho Jumapili watamalizia wikiendi yao ukumbi wa Dar Safari Buza Dar.

**Twanga Pepeta**
Jana Ijumaa walikuwa ndani ya ukumbi wa Diamond Jubilee katika onyesho maalum, leo Jumamosi wapo Nsala Lounge Mbezi Kwa Yusuph, kila Jumapili wapo Gwambina Lounge (zamani TTC Club Chang'ombe).

**Waluguru Original**
Bendi hii inafanya shughuli zake mjini Morogoro, hutoa burudani kuanzia Alhamisi katika ukumbi wa Didi's Break Point Iringa Road, Ijumaa ndani ya ukumbi wa Kambarage SUA, Jumamosi wapo Terminal Pub Msamvu na Jumapili wapo eneo hilo, katika ukumbi wa F2 Florida.

**Kimokimo Band**
Kundi hili ambalo linaongozwa na mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa inatoa burudani ya nguvu katika ukumbi wa Mariot uliopo enep Extertanal.



MSONDO

## BARIZI LA PWANI



# SHAKIRA SAIDI-2

## Mwimbaji mkongwe wa taarabu, mwenye sauti tamu ya kinanda

JINA lake halisi ni Tatu Said, lakini wengi wanamfahamu kama Shakira Said kutokana na kuwa na umahiri mkubwa wa kuimba muziki wa taarab.

Mkongwe huyu wa muziki ambaye sasa ni marehemu sehemu kubwa ya maisha yake yalitawaliwa mkoani Tanga, huko ndiko alikozaliwa, kuolewa na kuingia katika fani ya muziki.

Katika sehemu ya kwanza tulijikita katika kumuangalia makuzi na jinsi alivyoanza kuingia katika muziki wa Taarab, leo tunaendelea kusimulia jinsi alivyozidi kujizatiti katika muziki huo hadi akajizolea umaarufu.

Akiwa katika maisha ya muziki wa taarabu, wapenzi na mashabiki wa wakati huo walilinganisha na sauti ya Tatu Saidi kuwa haitofautiani sana na ya Shakila, na hivyo wakampachika jina hilo

Shakila Said alikuja kuwa miongoni mwa waanzilishi wa kundi la taarabu la Black Star, huko alionyesha cheche zake baada ya kuachia tungo yake ya "Duniani nakupenda wewe".

Aidha, alifanikiwa kuimba wimbo mwingine unaoitwa "Jogoo acha makuu", ukishirikiana kuimba na mwimbaji Hamadi Mrisho.

Wakati huo wimbo huo uliwavutia mashabiki wengi na hata walipokwenda kwenye kumbi, watu walijaa pale Black Star ilikuwa ikitoa burudani.

Inaelezwa kuwa kupendwa kwa wimbo huo ilitokana na uwezo mkubwa wa Bi. Shakila kuweza kucheza na sauti katika nyimbo za taarabu.

Katika kipindi cha mwaka mmoja Shakira, alifanikiwa kuimba nyimbo kali kama vile Kitumburi, "Macho yanacheka" na "Kifo cha mahaba".

Hapo ndipo umaarufu wa Black Star ulipozidi kusambaa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, huku sauti yake ikisikika kila wakati katika vituo vya redio na kwenye kaseti kwenye nyumba za watu.

Shakira aliitumikia Black Star kwa miaka kumi, kuanzia 1961 mpaka 1971, baadaye alihama.

Akihojiwa na chombo kimoja cha habari Shakira alinukuliwa akisema "Nikiwa Binti wa umri wa miaka 18, niliondoka Black Star baada ya kutumikia kwa kipindi kifupi, nikaenda kujiunga katika kundi la Lucky Stars lililokuwa mjini Tanga,"

Shakila akiwa katika kundi hilo alifanya maajabu kwa kuimba nyimbo nyingi zenye maudhui maridhawa kwa jamii.

Baadhi ya nyimbo hizo ni pamoja 'Mapenzi ni kama donda', 'Mapenzi Yamepungua', 'Bunduki bila Risasi', 'Viva Frelimo', 'Kitanda Kuwekwa Pembeni' na nyingine nyingi.

"Nilianza muziki mwaka 1960 kabla ya nchi yetu haijapata Uhuru na nimekuwa huko kwa miaka mingi. Wakati nikianza muziki, nilimkuta marehemu Saada Binti Saad na Fatuma Binti Baraka 'Bi Kidude," alisema Shakira.

Maisha yake ya ndoa msanii huyo aliingia akiwa na miaka 11 kwa kuolewa na mume wake wa kwanza.

Katika ndoa yao waliweza kupata mtoto mmoja, lakini ndoa hiyo haikudumu waliachana.

Shakila aliolewa tena na mume mwingine aliyepata naye watoto watano.

Kwa bahati mbaya mnamo mwaka 1975 mume huyo alifariki baada ya miaka 18 ya ndoa yao.

Hata hivyo, aliolewa na mume mwingine ambaye walipata watoto watano, huyo naye waliachana.

Aliolewa kwa mara ya nne na kubahatika kupata watoto wawili.

Hata hivyo aliipokuwa na mimba ya mtoto wa mwisho mwaka 1993, aliachana na mume wake.

**Itaendelea wiki inayokuja**

# 50 CENT YAMKUTA




KWELI uzunguni si uswahilini! Kwani kibongo bongo ni suala lisilowezekana pale mtoto wa kiume tena mwenye umri wa kuoa kutangaza hadharani kwamba baba yake hampatii pesa za matunzo kama mtoto.

Na endapo akionekana mtoto wa aina hiyo, basi watu hawakawii kumpachika majina kama kama 'mtoto wa mama', 'mtoto laini' au 'mtoto nyanya' kutokana na tabia yake ya kutojiweza kuhimili mitikisiko ya maisha na badala yake anataka vitu rahisi bila kufanya kazi.

Lakini kwa wenzetu Marekani jambo hilo hakuna, kwani kisa cha hivi karibuni mtoto wa kwanza wa 50 Cent, Marquise Jackson mwenye umri wa miaka 25, anadai kiasi cha pesa alichopokea kila mwezi kama matunzo ya mtoto kutoka kwa baba yake hakikutosha.

Hivi majuzi, Marquise Jackson alienda kwenye Instagram Live na mjasiriamali na rapa wa zamani Choke No Joke, na kuelezea kusikitishwa kwake jinsi baba yake anavyompatia malipo ya matunzo yake.

Kulingana na maelezo yake alieleza kuwa baba yake yaani 50 Cent analipa dola 6,700 sawa na sh milioni 15. 6 kwa mwezi



Marquise

hazimtoshi kumudu maisha aliyodai kuwa alihitaji katika jiji la New York.

Kama anavyoonekana kwenye video akiongea amesema kuwa baba yake yupo katika orodha ya watu matajiri, lakini yeye mtoto wake anapewa kiasi hicho ambacho akimtoshi kuishi.

"Unamzungumzia mtu ambaye yupo katika orodha ya Forbes, unazungumza juu ya mtu ambaye ana tatizo na kila mtu, huwezi kuishi katika kitongoji chochote kwa dola 81,000 kwa mwaka sio pesa nyingi. Huwezi kuishi popote. Unazungumza juu ya mtu ambaye ana mgogoro na kila mtu kwenye tasnia, huwezi kuishi popote." amesema

Hata hivyo, Choke No Joke aliingilia kati kwa kumwambia Marquise ikiwa baba yake anaweka milioni 15 kwa mwezi katika malipo ya msaada wa mtoto, basi mama yake pia Shaniqua Tompkins, anapaswa kuongeza nusu nyingine, na kufanya apate milioni milioni 30.

Licha ya maelezo hayo ya Choke, Marquise aliendelea kudai kuwa pesa hizo hazimtosha. kuishi katika jiji la New York.

Choke alimwambia mtoto huyo wa 50 Cent kuwa lazima uache kulinganisha watu.

"Unajilinganisha na wewe kaka. Unalinganisha na kiwango chako cha maisha. Huwezi kufanya hivyo."alisisitiza na kuongeza "Ninajua jinsi unavyohisi kutokuwa na kitu, mfano mimi Niliondoka kwenye nyumba yangu iliyoungua nilibaki Sina kitu.imagine Ilinibidi nijenge upya maisha yangu kwa dola 6700 hiyo hiyo ambayo unaiona ndogo kwa mwezi."



50 Cent



# Davido, Chioma kama kawa

HATIMAYE mwanamuziki wa Nigeria, Davido na mchumba wake Chioma wameendelea kuonyesha dalili ya kurudiana baada ya kuonekana hivi karibuni wakiwa pamoja.

Hata , bado bado haijaeleweka kama wawili hao wamerudisha penzi lao upya baada ya kutengana kwa muda mrefu licha ya kuwa na mtoto mmoja.

Wawili hao walionekana hivi majuzi kwenye video ambayo ilisambaa mitandaoni. Wote wawili walionekana wakiwa na wakati mzuri, huku Chioma akishangilia na kukumbatiana na Davido kwenye kilabu walipokuwa wakicheza na wimbo wake.



## Teni mbona huna shukurani?

MWIMBAJI wa kike wa Nigeria, Teni amekosolewa vikali na mashabiki zake baada ya kuonekana akipokea tuzo kutoka kwa Rais Buhari, huku akiwa hana tabasamu usoni.

Katika tuzo hizo za kitaifa wanamuziki wengine waliopewa ni Burna Boy na 2Baba.

Katika video fupi iliyosambaa mtandaoni ameonekana Teni akipokea tuzo kutoka kwa Buhari bila kuwa na tabasamu na hata alipoondoka alikuwa amekunja uso jambo lililowakera watu.

## Harryson mshukuru Mungu wako

MWANAMUZIKI nyota wa Nigreria, Harryson, amewapa furaha mashabiki zake baada ya kutangaza kwa sasa yuko huru baada ya kukamatwa na polisi.

Muda mfupi baada ya kuachiwa huru, Harrysong aliandika katika ukurasa wake wa Twitter kuomba maombi maalum ya upendo kutoka kwa mashabiki wake.

"Tafadhali niombeeni popote ulipo. Maombi tu, yenye upendo." Ameandika Harryson.





## Lala salama Rico Swavey

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Nigeria, Patrick Fakoya maarufu kama Rico Swavey, amefariki dunia baada ya kupata ajali mbaya ya gari.

Rico ambaye alishiriki shindano hilo awamu ya tatu, amefariki muda mfupi baada ya gari alilokuwa akilitumia kupata ajali na kumsababishia majeraha makubwa.

Kulingana na mshiriki mwenzake, Tobi Bakre amefahamisha kwamba amepata mshtuko baada ya kupata taarifa hiyo mbaya.

## Ushauri wa Temitope umeeleweka

MWIGIZAJI chipukizi wa Nollywood, Temitope Hamzat, maarufu kama 'BSOLUTION', amesema kuwa kukata tamaa kwa baadhi ya mastaa katika fani hiyo imesababisha kujiingiza katika ngono kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya familia.

Hamzat, amesema ni muhimu kwa waigizaji chipukizi kuwa na nidhamu, umakini, taaluma na kucheza kwa kufuata sheria za tasnia hiyo.

Mwigizaji huyo anayetoka jimbo la Oyo, amekaririwa hayo wakati akichangia mawazo yake kuhusu ngono kwa ajili ya majukumu katika tasnia ya filamu.



## Wahenga waliounda mifumo ya nchi na Nyerere

# Msekwa: 'Vijana, mkisikia TANU ni sisi'

**Na Anil Kija**




MOJA ya nahau za wahenga zilizopata kusikika ni Indira Gandhi, Waziri Mkuu wa zamani wa India ambaye alikuwa binti wa kiongozi mkuu wa India kuelekea uhuru, Jawaharlal Nehru. Nje ya Nehru kulikuwa na mpigania haki Mahtama Gandhi, ambaye hakutaka uongozi au utawala, akiwakilisha hisia za matabaka ya chini na watwana, licha ya kuwa mwanasheria aliyetokea Afrika Kusini akahamia India.

Indira Gandhi alirithi mikoba ya baba yake, na ni mmoja wa viongozi wenza muhimu wa 'Nchi za Kusini,' vuguvugu aliloongoza Mwalimu Nyerere miaka ya mwisho ya uongozi wake na halafu akaendelea katika kustaafu.

Gandhi alisema katika dunia (ya uongozi au utawala) kuna watu wa aina mbili, wanaofanya kazi (kwa bidii, au kwa nguvu zote kimyakimya) na wanaochukua sifa. Ni kawaida katika maisha kuwa mkuu wa shughuli fulani ndiye atakayejulikana na kusifiwa. Wengine ni wasindikizaji tu hata wangekuwa wameshiriki kwa kina kiasi gani katika 'kupika na kuopoa' hicho kinachosifiwa, hawawezi eti wajitokeze waeleze wanahusika vipi. Kugawa sifa ya mkuu wa kitengo, shughuli fulani ya pamoja au ya kiutawala ni aina ya uasi, kwa kushindana na huyo mkuu.

Ndicho alichosema Gandhi kuwa dunia ina watu wa aina mbili, wanaofanya kazi na wanaopokea sifa - akishauri kuwa yeyote yule ajifunze kubaki katika kundi la pili kwani hakuna msongomano huko. Ukitaka sifa unaweza kuumia kwani mara nyingi mtu anakuwa hajajiandaa kwa 'purukushani' ya kutafuta sifa hizo. Kwa jumla hakuna muda wa kutosha katika maisha kurudi nyuma na kutafuta 'ukweli' wa kila jambo. Historia inajazia tu kwa kumbukumbu za hapa na pale, hadithi.

Ndiyo maana kuna mtiririko wa historia hapa nchini kuhusu kilichotokea nchini hadi kufikia uhuru (kwa baadhi ya wachambuzi au wahakiki), kwa mfano historia ya Abdulwahid Sykes na uhusiano wake na Mwalimu Nyerere na wazee wa TANU, hasa waliotokea pwani, kuanzia Dar es Salaam, Bagamoyo hadi Rufiji. Wako wengine wa mikoa tofauti ambao umuhimu wao uliongezeka wakati wa uhuru hasa baada ya mifumo ya utawala na katiba kuundwa, hadi kufikia mwaka 1965 wakati wa kuunda 'demokrasia ya chama kimoja.' Kwa wale wa kwanza, hicho ni kipindi cha uzeeni kwao, kwani wanafuatilia mtiririko wa matukio hadi 'kunyang'anywa' chama chao.

Uko upande mwingine ambao ulihusika siyo na kukua kwa TANU kuanzia mwaka 1953 au kabla ya hapo, na kumkaribisha Mwalimu Nyerere (wakati huo ni mwalimu Julius na baadaye Mwalimu Nyerere kwa maana ya kufikia ngazi tofauti kama kiongozi mkuu wa nchi, tena kwa muda mrefu). Hawa walianza kuwa karibu na Mwalimu wakati uhuru unakaribia, hivyo Nyerere akawa anahitaji kuunda siyo tu taasisi bali mifumo, na ndiyo hapo wanaingia wasaidizi muhimu, nje ya wale ambao walipewa nafasi muhimu za uongozi, mmoja wao akiwa ni Rashidi Kawawa.

Wako wengine kama Pius Msekwa, Adam Sapi Mkwawa, Saidi Maswanya, Peter Kisumo, Chifu Abdallah Fundikira, au wasaidizi wa ndani kama Joan Wicken, Joseph Butiku. Dickson Nkembo au Timothy Apiyo, makatibu wakuu wa mihula ya kwanza.

Kielelezo cha nafasi za ushauri bila kushika nyadhifa muhimu zaidi ila baadaye ni Pius Msekwa, ambaye ni mmoja wa washauri wakongwe wa Mwalimu ambao bado wapo. Ni mtu 'anayetafuta elimu hadi China,' kwa msemo mwingine wa wanazuoni akiwa amestaafu, alifuatilia masomo ya shahada ya sheria (Chuo Kikuu Huria). Ni kuongezea shahada ya pili ya taaluma ya siasa UDSM akiwa Makamu Mkuu wa Chuo hapo Mlimani mwaka 1970-1976, halafu kutunukiwa nafasi ya profesa wa heshima wa taaluma ya siasa katika idara hiyo miaka ya baadaye. Hakuwa anahitaji shahada nyingine lakini ilimsaidia kufuatilia historia ya sheria zilizotungwa nchini, kwa upande mmoja akiwa mshiriki, na kwa upande mwingine akiwa raia, na ndiyo maana alitaka kujua kwa undani zaidi mtiririko wa sheria.

Nafasi ya Msekwa ilikuwa ya kipekee ambayo kwa njia tofauti iliendana na kijana wa baadaye, Samuel Sitta, kama washauri na wasimamizi wa taasisi ambao wao wenyewe walikuwa vyanzo vya sheria, Msekwa wakati wa awamu ya kwanza kwa masuala ya katiba na itikadi, Sitta kuanzia miaka ya mwisho ya Mwalimu hadi awamu ya nne, yote.

Mwaka 1958 Msekwa aliteuliwa katibu wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO) akiwa kama mwakilishi maalum wa Mwalimu, msaidizi maalum, halafu mwaka 1965 akawa katibu na jopo la kuanda mfumo wa uchaguzi katika 'demokrasia ya chama kimoja.' Ndiyo eneo alilofanyia kazi kuifikia shahada ya pili kwa tungo akiwa VC pale Mlimani, na kazi yake imekuwa rejea muhimu sana.

Mwaka 1976 akiwa bado Mlimani alipewa jukumu kwa kushirikiana na Sheikh Thabit Kombo (kiongozi mkuu wa Afro-Shirazi kuacha Sheikh Abeid Karume) kuunda mfumo wa chama kimoja (kuunganisha vyama) ambayo ndiyo hakikisho la msingi ya kuimarisha muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Yeye alikuwa katibu wa jopo kama ilivyokuwa mwaka 1965 ambako Kawawa alikuwa mwenyekiti. Unaweza kusema kuwa kazi yake ya ushauri na kusaidia kuunda mifumo ya nchi ilifikia tamati hapo, kwani nafasi za ukuu wa mkoa, katibu mkuu CCM au Spika wa Bunge hazikubadilisha lolote. Hakuwa tena katika nafasi hizo za ushauri na kuleta mageuzi.

Kama kielelezo tu, Samuel Sitta alikuwa mmoja wa walioandamana kupinga amri ya kuingia Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 1966, wakafukuzwa chuoni UCD na halafu baadaye kurudishwa. Lakini mwaka 1967 Mwalimu alipotangaza kutaifisha mali kuu za wageni, kundi lililompinga wakati huo likageuka kuwa maswahiba wakubwa kwa kuwa ndio walipewa majukumu ya kusimamia sekta ya umma. Eneo hilo likawa sehemu ya sintofahamu za kisera kwa mfano mashirika kupata hasara, au eneo la sekta binafsi na sekta ya umma.

Kielelezo cha nafasi ya Msekwa na makada wengine wa ngazi za juu CCM (au TANU kabla) ni kilichotokea akiwa Mlimani miaka ya 1970. Kuna hadithi kwamba wakati mmoja Msekwa aligombana na uongozi wa Umoja wa Vijana wa TANU Mlimani, wakamwambia wataenda kumshtaki TANU. Inamaanisha wangemwona katibu mtendaji wa kipindi hicho, asiyekuwa kabisa na historia ya Msekwa katika chama. Hadithi inasema aliwaangalia wale vijana akawaambia 'vijana, mnaposikia TANU ni sisi.' Ina maana ili achukue hatua dhidi ya Msekwa, ingebidi kwanza Mwalimu aombe ushauri wa Msekwa -ni kichekesho wasichokijua viongozi wa vijana UDSM.

Ni mazingira tofauti kabisa na alichojibu Makamu Mkuu wa Chuo, Ibrahim Kaduma (sasa marehemu), kada wa TANU aliyepelekwa Mlimani kama VC mwaka 1977 kuchukua nafasi ya Msekwa ambaye baada ya hapo alihamia CCM kama katibu mtendaji, Nyerere akiwa mwenyekiti wa chama. Kaduma alikuwa katibu mkuu Hazina, akawa mkereketwa anagombana na wakuu wake (mawaziri), akahamishwa kusimamia Idara ya Taaluma za Maendeleo (IDS) ambako mwaka 1975 alijituma kufanya kampeni na kupeleka vipeperushi vya 'tumia kura yako vizuri, mchague Nyerere' akiwa hana mpinzani, ila giza. Ni zile kura za ndiyo na hapana za demokrasia ya chama kimoja kwa nia ya kuwaongoza wananchi nani anafaa kwa nafasi hiyo, tofauti na ubunge.

Aliteuliwa Waziri wa Nchi kwa Mambo ya Nje baada ya uchaguzi Oktoba 1975 na kukaa japo kwa Februari 15, 1977 Mwalimu alipomteua mtu wa karibu zaidi, Benjamin Mkapa, kwa nafasi halisi ya uwaziri wa Mambo ya Nje. Kaduma alirudi UDSM kama VC badala ya Msekwa, na wakati akipambana na vijana wale wale wa chama Mlimani, wakatishia kumshtaki (wakati huo CCM imeundwa tayari) aliwajibu kuwa 'damu ya CCM inapita katika mishipa yake.' Yaani watajifunza huko nini itikadi ya CCM endapo wataenda kupeleka mashtaka dhidi ya kada huyo!

# Manufaa harakati za Nyerere, TANU kabla, baada ya uhuru

Na Dk. Kamugisha Byabato

HISTORIA ya Tanzania inahusiana na maisha ya Baba wa Taifa letu, Mwalimu Nyerere, tangu na kabla ya Uhuru. Wakati wa uhuru, na uongozi wake na hata mpaka sasa, baada ya kung'atuka madarakani na kutangulia mbele ya haki, sera na itikadi zinaendelea kugusa maisha ya wengi nchini na hata dunaini.

Kwa kifupi ana mengi, na haiwezekani kuwasilsha yote, bali kuushia baadhi ya vipengele. Hivyo, inapoangaliwa katika eneo la vijana na watoto kuanzia zama Tanganyika na baadaye Tanzania katika mfumo wa elimu, wana mengi wamefaidika nayo.

Mimi nikiwa mzaliwa wa mwaka 1955 katika kijiji cha Kishanje, Tarafa ya Bugabo, Wilaya ya Bukoba Vijijini. Baba yangu alikuwa dereva aliyepatia ujuzi huo katika Vita ya Pili ya Dunia, alikohudumu katika majeshi ya Uingereza .

Hapo alipitia Kenya, Afrika Kusini, Madagascar, India Ceylon (sasa Sri Lanka hadi Burma (sasa Myanmar). Baada ya vita hivyo, askari Aba Yangui na wenziwe walirudi kwao, Tanganyika na nchi nyingine za Afrika zilizokuwa bado makoloni ya nchi za Ulaya.

Ni kipindi hicho walikuwa na moto wa kuondoa utawala wa kikoloni kwa kudai Uhuru, katika zama Mwalimu Nyerere alijiunga nao katika harakati hizo.

Kwa hiyo, ingawa nilizaliwa wakati wa ukoloni, lakini nilikuwa katika familia ya wanaharakati wa mapambano ya kudai Uhuru, baba yangu akiwa kiongozi wa TANU katika eneo lake la Bugabo.

Nikiwa mdogo, nilikuwa naona shughuli mbalimbali kwetu nyumbani na kusikia habari mbalimbali kuhusu siasa na mapambano ya kudai uhuru.

Kwetu walikuwa wageni hawaishi, hasa vijana wa TANU Youth League (TYL), wakifanya maandamano na nyimbo, wakiongozwa na Bwana "Kanchaka". Pia kwetu walikuwa wanakuja na wazee rika la baba, kina Edward Barongo, Ali Migeyo (Ali Matata), John Kami, na wengineo.

Nilikuwa nasikia simulizi juu ya mbinu za utawala wa kikoloni kuchelewesha Uhuru kwa kuanzisha vikundi kinzani vya UTP na Congress, utaratibu wa kura ya mseto ya kila mtu kuchagua watu watatu (Mweusi, Mhindi na Mzungu), na mambo kama hayo.

Ulipotimu wakati, shamrashamra za Uhuru na Jamhuri ya Muungano mwaka moja baadaye. Katika shughuli hizo zote, jina la Mwalimu Nyerere lilikuwa haliishi kutamkwa na maandalizi ya mikutano yake au ya wanasiasa wengine wa TANU yalikuwa yanafanyika kwetu nyumbani.

Pia, nilikuwa naona na machapisho mbali mbali yakiwemo magazeti na vijarida, vilivyohusu mapambano na matayarisho ya Uhuru, ingawa nilikuwa bado sijajua kusoma.



Wanafunzi wakiwa shuleni.



Shule ya Msingi Mwisenge, Butiama, alikosoma Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### ELIMU BAADA YA UHURU

Sera za Elimu za Mwalimu Nyerere, zilianza kunihusu pale nilipoanza shule. Tanganyika ilipopata Uhuru, ilirithi mfumo wa elimu uliokuwa umeandaliwa na wakoloni, uliosisitiza mtengano wa watu kwa misingi ya ubaguzi wa rangi, makabila, dini na hata matabaka ya watu au maeneo fulani fulani hata ndani ya kabila moja.


Kulikuwapo shule za watoto wa Wazungu, watoto wa Wahindi, watoto wa machifu na hata watoto wa matajiri. Shule nyingi ziliendeshwa kwa mfumo wa usimamizi wa madhehebu ya dini, hata zile mbazo hazikulenga kuzalisha viongozi wa dini.

Pamoja na hayo, shule zilikuwa chache na mara nyingi mbali na makazi ya watu waliokuwa wengi. Shule za bweni zilikuwa chache na mara nyingi watoto walilazimika kuishi katika familia za watu waliokuwa karibu na shule chache hizo.

Bado ubaguzi uliendelea kuwapo kwa misingi ya kiuchumi, kwani licha ya kuwa na uhuru wa kinadharia kwa mtoto yeyote kusomea shule yoyote, bado kulikuwa na vikwazo vya gharama za ada ya shule, sare, usafiri na chakula na uwezo wa wazazi kumudu gharama hizo.

Pia, shule ziliendelea kuwa chache na mfumo wa elimu uliendelea kusimamiwa na madhehebu ya dini, ingawa zilikuwapo shule chache zaidi za serikali tangu ukoloni. Ingawa sasa watoto wote waliruhusiwa kuingia na kusoma katika shule za madhehebu yote.

Wazazi wengi wa nyakati hizo, walipendelea watoto wao wasomee katika shule za madhehebu yao, labda kwa wale tu ambao madhehebu yao hayakuwa na shule katika maeneo husika.




Uboa wenye orodha ya watu maarufu waliopitia shule

Baada ya Uhuru kukapatikana sera ya serikali, hapo ikabadilika kuondoa ubaguzi wa rangi katika mfumo wa elimu na kuruhusu watoto wa dini zote kusomea katika shule walizozipenda.

Nakumbuka, kadri ya maelezo ya Mwalimu Benedict Bingileki, mmojawapo wa walimu wangu mashuhuri katika shule ya msingi, alisema kuwa mpangilio wa matamshi ndio uliokuwa pia mpangilio wa vipaumbele katika mapambano na maadui hao.

Mapambano dhidi ya Ujinga yalipewa kipaumbele kwani nchi isingeweza kupambana na umasikini wala maradhi bila ya kupambana na Ujinga

Kwa hiyo, sera ya serikali ilitilia mkazo zaidi kufuta Ujinga, kwani ndiye aliyeonekana kama kinara wa maadui wetu hao watatu.

Kabla ya Uhuru mfumo wa elimu ulikuwa ni miaka minne ya Shule ya Msingi (Primary School na baadaye Lower Primary School) ikifuatiwa na miaka minne Shule ya Kati (Middle School) baadaye 'Upper Primary School', ikifuatiwa na miaka miwili ya sekondari na miaka miwili tena ngazi hiyo ya sekondari, kila hatua ilikuwa na mtihani mkuu wa mchujo.

Hivyo, katika mfumo, anasema kwanza, mabadiliko ya kwanza yalikuwa ni kurekebisha mfumo wa elimu kwa kupanua elimu ya msingi kwa kuongeza idadi ya shule, kufupisha mchakato wa shule ya msingi kutoka miaka nane hadi saba na kuziunganisha shule za msingi na kati (Lower & Upper Primary Schools) zikaitwa za msingi.

Mpambano huo ulitumia nyenzo mbalimbali, zikiwemo madhehebu ya dini, pia vyama vya ushirika na vyama huru vilivyokuwa na mlengo wa kukuza elimu.

Chama cha Wazazi, Tanganyika Parents Association (TAPA), kilichoanzishwa hata baadaye kilikuja kushirikishwa na TANU, sasa kipo kama Jumuiya ya Wazazi ndani ya CCM, ilisaidia kujenga na kuendesha shule za msingi na za juu na zile za Upili.

**• Mwandishi ni Mhandisi na Mhadhiri Mstaafu wa vyuo vikuu nchini na simulizi inatokana na uzoefu binafsi wa alichopitia maishani.**

MIAKA 23 YA NYERERE:

# Butiku ataka jukwaa la maadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



MWASISI wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, ametimiza miaka 23 tangu alipofariki dunia. Kiongozi huyo alifariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London nchini Uingereza alikokuwa akipatiwa matibabu.

Katika harakati na uongozi wake alikuwa mtu wa kusimamia maadili, utu na uzalendo kwa taifa. Pamoja na kupita miaka mingi tangu kufariki mwaka 1999, fikra na matendo yake bado yanaishi.

Hivi karibuni kumekuwa na kelele nyingi kuhusu ukosefu wa maadili na malezi, jambo ambalo ni ishara tosha kuwa taifa linapaswa kujitafakari katika kumuenzi Nyerere.

### JUKWAA LA MAADILI

Msaidizi binafsi wa Mwalimu Nyerere wa masuala ya utafiti, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Mzee Joseph Butiku, akizungumza kwenye mjadala wa kitaifa wa wazee jijini Dodoma mwanzoni mwa mwezi huu, alisema ni wakati sasa wa kuwa na jukwaa la maadili la taifa ambalo wazee wanapaswa kuliunda.

“Taasisi ya Mwalimu Nyerere tunakusudia kuunda kwa kuwa wazee ndio msingi wa jukwaa hili, ili kueleza vijana, tutakuja kwenu (wazee) tupate maoni yenu kwa ajili ya jukwaa la uzalendo, tusipokuwa na tabia ya kutekeleza ni kazi bure.

“Kama huna serikali makini ni bure, kama una wazee waoga ni bure, kama una wazee wanasimangasimanga serikali ni bure. Jukwaa hili litasaidia kuongoza taifa vizuri kuwa watu Watanzania,” anasema.

Kwa mujibu wa Butiku, vijana wanatakiwa kuwa kama Mwalimu Nyerere katika kuheshimu wazee wao na kusimamia utu na haki sawa kwa wote.

“Shida yetu wote ni tabia, wazee simamieni tabia bila kuogopa, sasa hili kundi la wazee uzee ndio watu, misingi inasimamiwa na wazee, tunataka wazee wanaosimamia misingi, tumeshindwa kusimamia misingi,”anasema.

Anasema “Tumeshindwa kulea, tumemsikia mama Samia(Rais Samia Suluhu Hassan) anasema njooni tushirikiane tulee, tunashindwa tunakabidhi polisi wanakurupushana na panyaroad, piga hao nyie mnashukuru, hivi ni binadamu gani wanatengeneza bunduki kuua watoto wao, wameshindwa nini?”.

“Wale watoto msiwalaumu ni sisi, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, nani kawalea hao? katika mfumo wetu wa Afrika, tunasema huyu binti wa nani ana tabia mbaya, huyu kijana wa nani hastahili kuwa hivyo, wote tunajua amekosea kwa sababu ule mfumo wa maadili tunaufahamu wote tumefundishwa.

“Wale wanaoiba ni watoto wa nani kwa hiyo kazi nyingine yetu sasa ni kulea vijana bila kubabaisha, bila unyonge, Rais ni mtu, urais anatoa kwetu sisi wazee, wazee kwanza ndio watetezi wa misingi,” anasema.

Anahimiza malezi kwa watoto na kwamba taasisi inaona kuna umuhimu wa kuundwa jukwaa hilo.

“Wazee, vijana na watoto tuunde jukwaa la uzalendo litakalolinda misingi yetu, na sisi wazee tusimamie kulea watoto, tujue tufundishe nini wakati gani na vijana wetu watatusikiliza na madaraka tutawapa hatutataka kuwanyang’anya sisi ni washauri,”anasema.

“Wote tunalalamika tumeshindwa kulea watoto, tumemkabidhi kijana wetu mmoja anaitwa Mama Samia (Rais Samia Suluhu Hassan), tulimpa mdogo wetu, Magufuli (Hayati Rais John Magufuli) na mwingine alikuwa mdogo, Kikwete (Rais Mstaafu Jakaya Kikwete) sijui kama wote walikuwa wanatambua kuna watu wanaitwa wazee,” anaongeza.

Anasema katika kuchagua viongozi wazee wana kauli kubwa katika jamii huko wanaoitwa viongozi wa jamii.

“Mimi nataka kuwa Rais wa nani? Sina nguvu hizo, wazee wanataka kukaa kwenye mabaraza? Mbaki wazee, nchi ikishindwa ni nyinyi sio kwenda kutafuta vyeo vingine cheo cha maana ni cheo cha mzee simamieni, muulize Rais, Waziri kwanini hili haliendi vizuri.

“Kwa sababu tumechagua watu bungeni yupo mwanasheria wa serikali anasimamia katiba yetu kama kuna mapungufu kusahihisha ni rahisi na sio ubishi wa wazungu huko waliibiana mali wakajenga uhasama wa kudumu na leo ndivyo walivyo wanyang’anyi na wezi,” anasema.

Anasema wazee wakiwa waoga kusaidia vijana wasinyang’anywe watakuwa wamekwisha.

“Jukwaa la uzalendo msingi wake uchumi, mama anasema kilimo, viwanda, umeme, hayo ndo ya msingi, sisi tunasema katiba ipo, tukiacha wizi na kufundisha kunyang’anyana.

“Kama chuo kikuu kitatoa vijana ambao hawana tafsiri ya maisha ya leo kama walivyokuwa nayo kina Nyerere basi hatuna taifa, kama chuo hakitafundisha utu na watu na kujitegemea watafundisha watu waporaji walioelewa misingi ya wazee wao litakuwa taifa bora,” anasisitiza.

Butiku anasema dunia haiwezi kufundishwa kwa silaha bali kwa moyo wa upendo na kwamba amani,usalama, maadili na tabia kwa watanzania hilo ndilo taifa.

“Leo mahitaji yameongezeka Mwalimu Nyerere na wenzake walisimamia utu sawa, haki sawa kwa wote na ilikuwa misingi ya wazee wao, Katiba haijaandika ukiwa kiongozi ule rushwa au kunyang’anya mali za wenzako, wewe useme wazee wamepitwa na wakati hii ni tabia mbaya,”anasema.

Butiku anasisitiza kazi ya wazee ni kusimamia misingi ya utu bila kubabaika.

### VIJANA WAFUNDISHWE

“Ujamaa wa Mwalimu Nyerere ni kujihudumia mahitaji yetu, kuna kelele nyingi hakuna hela, Mungu ametupa akili tufanye kazi na kazi yetu ya msingi tangu mababu na mababu ni kulima kuwa na chakula.”

“Kwa kuwa tumestaraabika tulime kisasa na mazao yetu yaendelee katika viwanda na tuzalishe mahitaji yetu tutumie na mengine tuuze tupate fedha na tuwafundishe vijana wetu kazi,”anasema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Enzi za kutumia vyombo vya udongo kwa mgeni

## •Vinahifadhiwa kabatini bila kuguswa
## •Familia ni mwendo wa plastiki na bati

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA ya nyuma akinamama wengi walikuwa na tabia ya kununua vyombo vizuri na vya gharama ambavyo hawavitumii kwenye matumizi yao ya kila siku, badala yake wanasubiri wageni ndiyo vitumike.

Wadau wengi wamenitumia ujumbe mfupi wa simu kuomba wiki hii iwekwe mada hii kwani wamekuwa wakikumbuka enzi hizo walivyokuwa wakipigwa marufuku na mama zao kutogusa hata kabati lililowekwa vyombo hivyo, achilia mbali vyombo vyenyewe.

Ni kweli kabisa zamani akinamama hasa kwenye miji mikubwa hususan Dar es Salaam, walikuwa ni lazima wawe na kabati ambalo linakaa varandani. Linakuwa la vioo, na humo ndani mnakuwa na vyombo vya udongo na kioo na hasa wakati ule vinakuwa vinatoka Mashariki ya mbali, glasi na seti ya vijiko.

Vyombo hivyo vinakaa kwenye shefu moja la kabati ambalo watoto wanapigwa marufuku hata kuguswa.

Kwa muonekano vyombo hivyo vinavyoonekana vinakuwa kama ni mapambo, hivyo ni marufuku kuguswa.

Kinababa nao walionekana kuwaunga mkono akinamama kwa hilo, na sasa ikawa kama utamaduni fulani hivi ambao haukuwa rasmi.

Inawezekana wakati huo walikuwa sahihi kwani maisha na uchumi wa kipindi hicho miaka ya 1990 kurudi nyuma hayakuwa mazuri kutokana na sababu ile ile ya siku zote tunazozisema, athari za Vita vya Kagera, vyombo huharibika, kupasuka au kuchakaa.

Hali hiyo iliwalazimu kinamama kuhifadhi baadhi ya vyombo kwa ajili ya siku za matukio maalum kama siku za sikukuu, sherehe au wageni ili kulinda heshima ya familia.

Kutokana na hilo watoto wote nyumbani walikuwa wanatumia vyombo vya asili ya plastiki au bati, iwe kwenye chai au chakula, mwendo ni huo huo.

Watoto huviona vyombo vikitolewa siku wakija wageni tu, na vinatumiwa na wao tu, wakiondoka vinarudishwa tena pale pale, maisha yanaendelea.

Mtoto hadi anakuwa hajawahi kutumia au kukigusa chombo hicho. Kwa hali hiyo mara nyingi ilikuwa ikiwafanya wengi kukosa kujiamini na kuvivunja siku wanapoambiwa waoshe na hasa watoto wa kike.




Kwa sasa kuna mtu akisoma hivi hasa wa kizazi cha sasa anaweza kushangaa, kwani siku hizi wanakula tu kwenye sahani nzuri na za udongo bila matatizo yoyote.

Maisha yamebadilika sana, wazazi wa sasa wanajali zaidi watoto wao kuliko wageni, pia hata tabia ya kutembeleana kila Jumapili au mara kwa mara hakuna tena.

Watoto wa siku hizi wanajua vitu mapema, na si watundu sana kama wa zamani, pia vyombo vya udongo vipo vingine si vya gharama sana.

Na kwa kuthibitisha hilo, baada ya kuweka mada hii kwenye mtandao wa kijamii, wengi walioandika ni wale ambao walikutana na madhila haya, lakini kwa sasa wanapingana na tabia hii kuwa haina maana hata kidogo.

Wanakubali inawezekana kwenye mazingira ya miaka ya nyuma ilikuwa sahihi, ingawa wengine bado wanatilia shaka, lakini wengi wamesema hawawezi kuendeleza tabia hii kwa watoto wao. Sasa tuanze kuchambua yaliyoandikwa na wadau waliochangia mada hii. Kuna mmoja alisema mke wake alikuwa na tabia hii hata miaka ya hivi karibuni, inawezekana kwa sababu ya alivyozoezwa huko nyuma, lakini kwa sasa amebadilika.

"Mke wangu alikuwa na hiyo tabia, vyombo vya udongo kibao na glasi za kioo maridadi lakini anapakulia kwenye sahani za plastiki eti watoto watavunja. Nikamwambia mimi ndio ninenunua kama vinavunjika vivunjike tu nitanunua vingine, hilo povu lake nilichoka. Lakini sasa amebadilika."

Mdau mwingine naye akadai mkewe alikuwa na tabia hiyo, lakini akamwambia.

"Kwa maisha hata sioni wageni kuja kuzitumia hizo sahani, bakuli na vikombe, tusipoangalia tutakufa bila kuzitumia, akabadilika."

Mama mmoja aliandika jinsi siku alivyopewa kuosha vyombo vya udongo kwa mara ya kwanza.

"Mkuu umenikumbusha, enzi za utotoni unaosha vyombo mara paa sahani imevunjika kwa utelezi wa povu la sabuni, nikamsikia mama sebuleni akipaza sauti 'we vunja tu', kwa wasiwasi, kingine kikavunjika, akasema 'Yesu wangu huyu mtoto nammaliza leo, niliogopa maana mama alikuwa hachagui pa kupiga." Mchangiaji mwingine akaandika

"Hiyo staili ya kizamani sana wakati vyombo vya udongo vikiwa ni adimu sana sokoni. Kwa sasa itakuwa ni aibu kubwa kuweka sahani na vyombo vya udongo kabatini halafu familia inatumia vya kawaida."

Huyu mwingine ameshuhudia familia nyingi zamani zikiwa kwenye hali hiyo, hata ya kwao alipokuwa mtoto.

"Nimeshuhudia familia nyingi hata kwenye familia yetu yaani kabatini kuna vyombo vizuri na vipya kabisa kama sahani, bakuli,vikombe na vyombo tofauti vya matumizi ya kila siku lakini havitumiki na familia mpaka waje wageni, tena hata baba mwenye nyumba anaweza kuwekewa chai kwenye kikombe chanye ufa."

Mchangiaji huyu alisema kwao waliyabatiza majina sahani za pilau

"Kwa sababu sahani za udongo na kioo kwetu zilikuwa hazitolewi kabatini mpaka waje wageni au siku mama apike pilau mimi na ndugu zangu tukazibatiza jina tukaziita sahani za pilau."

Kuna huyu jamaa aliyetoa mpya, wazazi wake walivunja sahani za udongo

"Umenikumbusha mbali sana wakati tukiwa wadogo na ndugu zangu, kuna vyombo mama alikuwa amepanga mistari ile ya juu ya kabati vilikua haviguswi ukiviigusa mama 'atakutafuna.' Siku moja walipigana na baba wakaparamia kabati likaanguka vyombo vyote vikavunjika, sisi badala ya kusikitika tulicheka kwa sababu huwa hatuvitumii lakini leo vimevunjika, hatari wee mama hasira zote ziliishia kwetu."



**Tuma meseji 0716 350534**

# Mgomo wa wahadhiri Nigeria wamalizika

**ABUJA,** Nigeria

WAHADHIRI katika vyuo vikuu vya nchini Nigeria wamesitisha mgomo wa muda mrefu ambao walianza kugoma miezi minane iliyopita.

Pamoja na mambo mengine walikuwa wakidai fedha zaidi katika vyuo vikuu, vifaa na malipo yaliyoboreshwa.

Duru kadhaa za mazungumzo na serikali zilishindwa kutatua mzozo huo. Mwezi uliopita mahakama iliamuru wahadhiri hao kusitisha mgomo lakini muungano wao ukakata rufaa dhidi ya uamuzi huo.

Hata hivyo, mapema jana Chama cha Wafanyakazi wa Vyuo Vikuu (Asuu) kilitangaza kusitisha mgomo huo baada ya mkutano wa viongozi wake uliokaa usiku kucha.

Makamu wa rais wa muungano huo Chris Piwuna, alithibitisha kwa BBC kusitishwa kwa mgomo huo.

Masharti ya kusimamishwa hayako wazi mara moja. Muungano huo umewataka wanachama wake kurejea kazini Jumatatu wiki ijayo.

Mapema wiki hii muungano huo ulitoa dalili ya wazi ya kusitisha mgomo huo baada ya mkutano na viongozi wakuu wa bunge la Nigeria.

Hatua hiyo ya kugoma kwa miezi minane ilikuwa mojawapo ya mgomo mrefu zaidi wa wahadhiri wa vyuo vikuu nchini humo. Ulitatiza shughuli za masomo katika vyuo vikuu vya umma nchini humo, na kuathiri karibu wanafunzi milioni mbili.

Kusitishwa kwa mgomo huo kunakuja kuwa afueni kwa wanafunzi hao baada ya miezi kadhaa ya kusubiri. **BBC**

**Mapema wiki hii muungano huo ulitoa dalili ya wazi ya kusitisha mgomo huo baada ya mkutano na viongozi wakuu wa bunge la Nigeria.**

# Ukraine hakukaliki tena, mabomu yapiga kila kona

**KYIEV,** Ukraine

MASHAMBULIZI ya mabomu yanaendelea kwa siku ya tano mfululizo nchini Ukraine, mengi yakilenga miundombinu mbalimbali katika maeneo yote.

Hata hivyo, vikosi vya Russia vilifanya mashambulizi mabaya ya makombora katika mkoa wa Zaphorizhzhia. Gavana wa mkoa huo Oleksandr Starukh, alisema mashambulizi hayo yalisababisha kuzuka kwa moto katika miundo mbinu kadhaa.

Ikumbukwe Zaphorizhzhia ndiko kwenye kinu kikubwa zaidi cha nyuklia barani Ulaya.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskyy, alisema kamwe nchi yake haitoacha kupambana.

Katika hali yenye utata, Ukraine ilidai kuyakomboa maeneo yapatayo 600 katika mkoa wa mwezi mmoja uliopita, yakiwemo 75 katika mkoa wa Kherson.

Kama madai hayo yana ukweli, basi kunadhihirisha kuna changamoto inayokabiliana nayo Russia katika kuyadhibiti maeneo iliyoyanyakua.

**Kuwaondoa raia inakuja siku moja baada ya Ukraine kusema kuwa itayadhibiti tena maeneo yake katika eneo la kusini la Kherson.**

### Ukarabati wa daraja la Crimea

Mamlaka za Russia zimefahamisha kuwa ukarabati wa daraja la Crimea lililoharibiwa katika mlipuko wa mabomu siku ya Jumamosi iliyopita, utakamilika ifikapo mwezi Julai mwaka 2023.

Daraja hilo ni mradi muhimu katika utawala wa Rais wa Russia Vladimir Putin, liliharibiwa katika mlipuko ambao unadaiwa kufanywa na Ukraine. Baadhi ya maofisa wa serikali walisherehekea tukio hilo.

Wakati hayo yakiarifiwa, Russia imekubali kuwasaidia wakazi kuondoka katika eneo ambalo imelinyakua kinyume cha sheria, katika hatua za kukabiliana na mashambulizi ya Ukraine.

Kuwaondoa raia inakuja siku moja baada ya Ukraine kusema kuwa itayadhibiti tena maeneo yake katika eneo la kusini la Kherson.

Aidha, ofisa wa ngazi ya juu wa Umoja wa Ulaya ameonya kuwa jeshi la Russia litaangamizwa na nchi za Magharibi ikiwa litatumia silaha za nyuklia katika vita hivyo.

Kiongozi aliyewekwa na Russia katika eneo la Kherson kusini mwa Ukraine, Vladimir Saldo, alitoa wito kwa raia kuhama akitoa mfano wa mashambulizi ya kila siku ya roketi kwa kuendeleza vikosi vya Ukraine.

Aliwahimiza watu kujiokoa kwa kwenda Russia na akaomba msaada wa Russia kusaidia zoezi hilo.

Wito wake baadaye uliungwa mkono na Naibu Waziri Mkuu wa Russia, Marat Khusnullin katika ujumbe kwenye televisheni ya serikali. Ukraine inakanusha shutuma kwamba inalenga raia wake yenyewe.

Wanajeshi wake hivi majuzi waliteka tena baadhi ya maeneo ya kaskazini-magharibi mwa Kherson, wakikaribia mji mkuu wa eneo hilo.

"Serikali ilichukua uamuzi wa kujiandaa kutoa usaidizi kwa wakazi wa eneo la Kherson kuhama maeneo mengine ya nchi," alisema Khusnullin.

Kundi la kwanza la watu kutoka Kherson linatarajiwa kuwasili katika eneo la Rostov nchini Russia, alisema gavana wake Vasily Golubev kulingana na shirika la habari la serikali (Tass).

### Ukraine yaomba msaada

Maofisa wa Ukraine wamelitaka Shirika la Msalaba Mwekundu kufanya ziara katika kambi ya magereza yenye sifa mbaya katika eneo linalokaliwa na Russia mashariki mwa nchi hiyo.

Mkuu wa wafanyakazi wa rais wa Ukraine, Andriy Yermak, alilitaka Shirika la Msalaba Mwekundu (ICRC) kutembelea gereza la Olenivka liloko Donetsk ndani ya siku tatu.


"Hatuwezi kupoteza muda zaidi. Maisha ya binadamu yako hatarini", alitweeti.

Mwezi uliopita, Shirika la Msalaba Mwekundu lilijaribu kuingia katika kambi hiyo, lakini lilisema lilikataliwa na mamlaka ya Russia.

Gereza la Olenivka limekuwa chini ya udhibiti wa mamlaka inayoungwa mkono na Russia huko Donetsk tangu 2014, na hali inasemekana kuwa mbaya.

Mwezi Julai, makumi ya wafungwa wa Ukraine waliuawa katika mashambulizi ya roketi katika kambi hiyo, ambayo pande zote mbili zililaumiana.

Ukraine ilisema gereza hilo lilillengwa na Russia kuharibu ushahidi wa mateso na mauaji, lakini madai hayo yalipingwa vikali. **DW**



Mwanajeshi wa Israel akimuelekezea bunduki mwanamume Mpalestina asiye na silaha wakati wa mapigano kati ya walowezi wa Israel waliowashambulia Wapalestina katika eneo la maduka katika mji wa Huwara Ukingo wa Magharibi jana. **PICHA AFP**



# Mahakama yatupa ombi la Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAHAKAMA ya Juu nchini Marekani imetupilia mbali ombi la Rais wa zamani wa nchi hiyo Donald Trump, la kuingilia kati mvutano wake wa kisheria na shirika la upelelezi FBI.

Hatua hiyo, inatokana na msako uliogundua nyaraka za siri za serikali katika makazi ya Trump huko Florida. Trump aliitaka Mahakama hiyo kufuta uamuzi wa Mahakama ya chini na kumteua mwamuzi huru ambaye angelikagua nyaraka hizo za siri zipatazo 100 na zilizogunduliwa na FBI Agosti 8 mwaka huu huko Maa-Lago, jimboni Florida.

Kwa jumla shirika hilo la upelelezi liligundua na kukamata karibu nyaraka 11,000 katika makazi hayo na Mahakama inatathmini uhalali wa mashtaka ya uhalifu na iwapo Trump aliondoa nyaraka kinyume cha sheria wakati alipoondoka madarakani.

Hata hivyo, Trump na washirika wake wamekuwa wakilalamika kwamba upekuzi huo ulichochewa kisiasa.

HABARI PICHA

# SHEREHE ZA MAADHIMISHO YA KILELE CHA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2022 KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akiwapungia mkono wananchi wakati akiwasili kwenye Uwanja wa Kaitaba, mjini Bukoba, mkoani Kagera kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa jana. **PICHA ZOTE: IKULU**




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi mbalimbali pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Kagera katika Maadhimisho hayo.



Rais Samia Suluhu Hassan akivalishwa Skafu na Vijana wa Skauti baada ya kuwasili uwanjani hapo.



Vijana wa Halaiki, wakitumbuiza kwa kuonesha kazi mbalimbali wakati wa maadhimisho hayo.



Viongozi mbalimbali wakiwa kwenye uwanja wa Kaitaba, kushiriki maadhim-isho hayo.



Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa vyeti kwa wakimbiza mwenge Kitaifa.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia.

Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# Mtake Msitake-1

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwangwo**

***MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yalipopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.***




**Kibaya zaidi ni kwamba yoyote aliyeonekana kupinga alishughulikiwa. Liliundwa kundi kama sungusungu, kazi ilikuwa ni kukamata, kuadhibu, kumtesa na kumuua yoyote yule anayeonekana kidomodomo wa kutaka kuwazindua watu kuwa 'wamepigwa'.**

***********************************

"Nimekwambia wewe utaolewa na mimi."

"Sitaki."

"Nini, unaweza kunijibu hivyo mimi, tajiri yenu. Hata baba na mama yako wananiogopa, sembuse wewe kifaranga tu." Maneno hayo yalimaliziwa na kumsukuma aliyekuwa akikataa na kuanguka sakafuni.

Kilichofuatia ni kilio cha msichana huyo alionekana kukataa katakata kuolewa.

Baada ya kuona hakuna kitakachoendelea. Akawageukia wasaidizi wake waliowaagiza kwenda kumchukua kwa nguvu binti huyo.

"Hebu mrudisheni huko mlikomtoa, maana ananiletea uchuro hapa." Akang'aka kwa hasira.

Haraka walimtwaa na kutoka naye nje.

Kwa hasira alikwenda kujipweteka kwenye kochi akiwa peke yake. Akapiga ngumi hewani. Alikuwa hajawahi kukataliwa na mwanamke yoyote yule.

Kwa mbali alianza kuona inawezekana pesa au utajiri siyo kila kitu kwenye hii dunia.

Pamoja na utajiri na pesa zake lakini bado anakataliwa na msichana huyo ambaye ametokea kumpenda kati ya wote aliowaona kwenye kijiji kile.

"Nifanye nini?" Akajiuliza, lakini akakosa jibu.

Tangu alipofika kwenye kijiji hicho na kumuona msichana huyo amekuwa akijaribu kuwa naye karibu akimzoea, lakini msichana amekuwa akimkwepa.

Na hata zawadi za nguo mbalimbali, hereni, mikufu na zingine ambazo alikuwa akituma wasaidizi wake kwenda kumpa, alikuwa akizikataa na kuwaambia wazirudishe.

Alifikiria mbinu nyingine anayoweza kuifanya kumshawishi msichana huyo, lakini kichwa chake kiligota.

"Nimbake?" Akajiuliza, lakini wazo hilo aliliondoa mara moja.

Ni kwamba kwa hadhi aliyokuwa nayo, pesa na utajiri hakuwa mtu wa kulazimisha penzi kwa nguvu kiasi cha kubaka. Kwake hiyo anaiona ni hatua ya mwisho wa kushindwa, pia hakutaka kumuumiza binti huyo mrembo. Pia ingeweza kumletea matatizo kwa wanakijiji kwani hata pale walipo bado wana manung'uniko kutokana na kununua ardhi yao kwa njia ya kitapeli na kinyonyaji.

Ghafla aliamua wazo hilo kulitupilia mbali kwa sababu ana mambo mengi ya kufanya muhimu zaidi, na suala hilo atalifanyia kazi baadaye.

"Ngoja niliache kwanza, ila huyu binti ananipa tabu sana, ni mrembo sana. Tena huyu hapa ndiyo hana matunzo yuko hivi, akiwa kwenye himaya yangu si atakuwa kama malaika?" Akamaliza kuwaza.

***********************************

Mosha Usonzo alifika kwenye kijiji hicho akitokea Arusha ambako baada ya kupata pesa zake za madini alianza kuwekeza sehemu mbalimbali.

Kuna maeneo aliwekeza kwa haki, lakini sehemu zingine aliwaumiza wananchi na hasa sehemu ambazo viongozi wao wana tamaa ya pesa.

Alifika kwenye kijiji cha Maweni na kuwatia mfukoni viongozi wa kijiji hicho kilicho barikiwa ardhi nzuri yenye rutuba.

Akawapa rushwa na zawadi za hapa na pale, kiasi cha kukubali kukaa naye kikao cha siri na kukubaliana kumuuzia asilimia 70 ya ardhi kwa madai ya kuwekeza.

Awali waliambiwa kuwa ardhi hiyo inatakiwa na serikali kwa ajili ya kujenga zahanati, shule, kituo cha polisi na kliniki ya mama wajawazito.

Bila kujua hili wala lile wanakijiji walikubali kwani waliona watakuwa wamebarikiwa kuwa na kijiji cha kwanza kuwa na vitu vyote hivyo muhimu.

Wananchi walitoa ardhi bila kusita, tena kukawa na sherehe kubwa, watu wakala na kunywa, asilimia 30 ya ardhi iliyobaki wakagawana wananchi kwani waliambiwa kuwa serikali itakapojenga vitu hivyo, haitamaliza ardhi yote, na itakapobaki, basi itarudishwa tena kwa wanakijiji waendelee na shughuli zao za kijamii kama kawaida.

Ukapita mwaka bila kuona hata dalili ya ujenzi. Minong'ono ikaanza na baadhi ya wanakijiji wakaanza kuongea bila woga kuonyesha kutoridhishwa na hilo.

Viongozi waliokuwa mlungula na mwekezaji wakaa tena kikao, wakaona wawaongopee wanakijiji kwa kuwapa pesa kama wanakodisha.

Wakaingia kichwa kichwa wakakubali. Mwekezaji sasa akaanza kuwatumia wanakijiji hao hao kama vibarua.

Ujanja uliotumika ni kwamba aliwapa kila mtu pesa kidogo, halafu ni kama alikuwa amewarudisha kila mmoja ardhi aliyokuwa akiimiliki ili waendelee kulima, lakini mazao alikuwa akiyachukua mwenyewe na kwenda kuyauza Dar es Salaam akijipatia pesa nyingi na kuwalipa pesa ndogo.

Mwanzo hawakugundua lolote, lakini baada mwaka mmoja mwingine ndipo walipoanza kuona athari ya walichofanya.

Kibaya zaidi ni kwamba yoyote aliyeonekana kupinga alishughulikiwa. Liliundwa kundi kama sungusungu, kazi ilikuwa ni kukamata, kuadhibu, kumtesa na kumuua yoyote yule anayeonekana kidomodomo wa kutaka kuwazindua watu kuwa 'wamepigwa'.

Kundi hili katili lilisababisha wanakijiji wafate mkia na kutekeleza yale ambayo wanaambiwa.

Usonzo, ingawa ana nyumba yake aliyoijenga kijijini hapo, lakini hakuwa anakaa mara kwa mara, badala yake alikuwa akija tu kuangalia maendeleo ya kazi yake chafu.

********************************

"Enock, mwenzio jana nilikamatwa nikapelekwa kwenye nyumba ya Usonzo."

"Unesemaje Mary?" Enock alishtuka.

"Nimekuja kuchukuliwa kwa nguvu hapa nikapelekwa kwa tajiri."

"Kwa nini?"

"Mhh, kwani hujui kuwa ananitaka?"

"Kwani si anajua kuwa una mchumba?"

"We lile baba si unalijua? Linatumia utajiri wake kurubuni na kutisha wasichana."

"Sasa ikawaje?"

"Wee mimi tena, nimempa makavu huko huko, ooh mimi nakupenda nataka nikuoe, nikamwambia. wee nini? Sitaki nakwambia." Wakati akiongea hivyo Enock akaangua kicheko, halafu akamkatisha.

"Usinidanganye Mary, wewe yule Usonzo umemjibu maneno hayo akuache kweli na ukatili wote ule?"

"Unafikiri aliniacha? Kwanza ile nafika tu, akanishika nywele zangu hizi rasta akanivuta na kuanza kuniambia maneno hayo, eti we mtoto kwa nini kila siku nakwambia nakupenda, lakini wewe huonyeshi ushirikiano. Si unajua kila akiniambia nakataa, sasa naona amekasirika na anatumia nguvu. Sikuogopa wala nini, nikamwambia sikutaki, akanisukuma, nikaanguka chini pu, sikuinuka hadi kawaambia wanirudishe. Unajua aliona aibu nimemkataa mbele ya wasaidizi wake na mimi nilifanya makusudi."

"We Mary wewe, unajua unajiweka kwenye hatari, yule si mtu mzuri, ni mtesaji na muuaji."

ITAENDELEA JUMAMOSI

HABARI MICHEZO

# PHIRI, CHAMA MGUU SAWA KUISAMBARATISHA AGOSTO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, akisema wamejindaa vyema kuelekea mechi dhidi ya Premeiro de Agosto kutoka Angola, straika wa timu hiyo, Moses Phiri amewaonya wapinzani wao kutambua mtanange huo utachezwa 'machinjioni' kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Mgunda alisema, wataingia uwanjani kwa tahadhari na kamwe hawatabweteka kwa sababu wanahitaji kupata ushindi tena katika mechi hiyo ya marudiano.**

"Nina mechi ngumu Jumapili, haitokuwa mechi rahisi hata wachezaji wangu wanalielewa hilo, lakini pamoja na hayo tumeajindaa kisawasawa kwa ajili ya kufanya vyema ili tuingie hatua ya makundi," alisema Mgunda.

Naye Phiri, aliliambia gazeti hili wanafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa kila upande kwa sababu lolote linaweza kutokea ndani ya dakika 90 zilizobakia.

Straika huyo tegemeo kwa sasa wa timu hiyo ambaye amefunga katika mechi zote tatu alisema yeye na wachezaji wenzake wanajua umuhimu wa mechi hiyo, lakini uzuri kwao watakuwa kwenye uwanja wa nyumbani ambao mara nyingi ni mwiba kwa wapinzani wao.

"Nadhani maandalizi yanaendelea vizuri, kila mmoja kwenye timu yetu anajua umuhimu wa hii mechi na uzuri tunacheza kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa hata wapinzani wanajua hilo, ni mwiba kwao, hivyo tunawahitaji sana mashabiki ili waje kutuunga mkono ili kuturahisishia kazi ya kupata ushindi," Phiri alisema.

Mzambia mwenzake ambaye alifunga bao la kwanza kwenye mechi iliyopita na kutoa pasi kwenye bao la tatu, Chama alisema yeye binafsi yupo tayari kimwili na kiakili kwa ajili ya mechi hiyo, na mpaka sasa anaamini mechi haijamalizika licha ya kuwa mbele kwa mabao 3-1.

"Niko tayari kwa ajili ya mchezo unaofuata, naamini hata wachezaji wenzangu nao watakuwa tayari, muhimu ni kujua kama tunataka nini kwenye mechi hiyo, tumecheza mechi ya kwanza Angola tumejua matokeo, mechi haijamalizika na tuna kazi ya kufanya, tutaingia katika mechi hiyo tukijua nini tunatafuta," aliongeza.

Kiungo, Jonas Mkude, alisema hataki kabisa kuona yanajirudia yaliyotokea kwa Jwaneng Galaxy ya Botswana msimu uliopita ambapo waliwaondoa katika michuano hiyo.

"Tumejiandaa vizuri, kwa sababu yale yaliyotokea kwenye mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy kila mtu yalimuumiza, mwisho wa siku yale yamepita, ndiyo maana tunakwenda kucheza mechi hii tukiwa na tahadhari kubwa tukijua mchezo wa mpira chochote kinaweza kutokea, " Mkude alisema.

Chama alisema yuko tayari kimwili na kiakili akijua yeye na timu yake nini wanakitaka kwenye mechi hiyo.

## Mzamiru: Hatarudia makosa CAF

**Na Saada Akida**

KIUNGO mkabaji wa Simba, Mzamiru Yassin, amesema malengo ya timu yao ni kupata ushindi katika mechi ya marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Premeiro De Agosto kutoka Angola itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kusonga mbele kwa heshima.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Jumapili iliyopita mjini Luanda, Simba ilipata ushindi wa mabao 3-1, mshindi wa jumla wa mechi hiyo atafanikiwa kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mzamiru alisema watajituma zaidi kuhakikisha wanafanya vizuri na kutorudia makosa ya msimu uliopita ambapo walishindwa kufika hatua ya makundi katika michuano hiyo na kuangukia kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kiungo huyo alisema hamasa iliyoko katika kikosi chao kwa msimu huu ni kubwa kwa sababu kila mchezaji, kiongozi na shabiki anataka kuona wanafanya vyema zaidi ya walivyofanya msimu uliopita.

Aliongeza pamoja na kupata ushindi katika mchezo wa kwanza huko Angola, bado wanaamini mechi ya marudiano itakuwa ngumu kwa sababu wapinzani wao hawatakubali kupoteza mechi zote mbili.

"Malengo yetu kama klabu kwanza ni kufuzu hatua ya makundi, ni kweli tumepata ushindi mzuri ugenini na tunajua mchezo wa Jumapili utakuwa mgumu, lakini tumejipanga kutafuta matokeo mazuri na kutorudia makosa ya msimu uliopita," alisema Mzamiru.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wakifanya mazoezi kujiandaa kuikabili Uganda katika mechi ya kusaka mshindi wa tatu kwenye mashindano ya CECAFA u-17 yanayomalizika leo nchini Ethiopia. **PICHA: TFF**

## Kipanga yatarajia makubwa Tunisia

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAWAKILISHI pekee wa Zanzibar waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Kipanga FC waliondoka nchini na kufika Tunisia salama kwa ajili ya mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji wao, Club Africain, imeelezwa.

Club Africain itaikaribisha Kipanga katika mchezo wa marudiano utakaochezwa kesho huku timu hizo mbili zikiwa na kumbukumbu ya sare ya bila kufungana.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa Kipanga, Khamis Hassan, alisema matarajio yao makubwa ni kupambana na kuhakikisha wanasonga mbele katika michuano hiyo.

Hassan alisema, wachezaji wana hamasa kubwa tangu walipokuwa wakijiandaa na mechi hiyo ya marudiano na walipoondoka waliahidi wanakwenda kufanya vyema katika mtanange huo.

"Tunakwenda kupambana ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri ugenini, najua haitakuwa kazi rahisi lakini jitihada na hamasa pamoja na matumaini vyote vinahitajika," kocha huyo alisema.

## KMC, Mtibwa kibaruani Ligi Kuu bara

**Na Saada Akida**

MAJIGAMBO yatawala kutoka kwa makocha wa KMC FC na Mtibwa Sugar, kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimefanya maandalizi mazuri ya kiwango cha asilimia 90 kuhakikisha wanashinda mechi hiyo.

"Mechi ya mwisho hatukucheza vizuri na makosa tuliyoyaona tumeyafanyia kazi, kikubwa tunaenda kutafuta matokeo mazuri, tutaingia kwa tahadhari kubwa kwa ajili ya kupata pointi tatu za nyumbani," alisema Ahmad.

Naye Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Dickson Mbekya, alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi na wao wamejipanga kuingia dimbani kwa tahadhari zote kwa ajili ya kupata matokeo mazuri.

"Tumejipanga vizuri na tutacheza kwa tahadhari kubwa kuhakikisha lengo la kutafuta pointi tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo linatimia," alisema Dickson.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### GVARDIOL ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka beki wa kulia wa RB Leipzig, Josko Gvardiol, 20. Nyota huyo kutoka Croatia, aliyehusishwa kuhamia Chelsea msimu wa joto, mwezi uliopita aliongeza mkataba wa kusalia Leipzig hadi mwaka 2027. ***(Football Insider)***

#### NKUNKU ANUKIA CHELSEA

CHELSEA wanatarajia kukamilisha usajili wa mshambuliaji Mfaransa wa RB Leipzig, Christopher Nkunku, 24, kabla ya kuanza kwa fainali za mwaka huu za Kombe la Dunia . ***(Bild via Metro)***

#### DORTMUND YAWEKA NGUMU

CHELSEA wanataka pia kuilipa Borussia Dortmund euro milioni 100 kwa ajili ya kinda wa England, Jude Bellingham,19, lakini wakali hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wanataka angalau euro milioni 120. ***(Bild)***

#### LAZIO YAIBANIA UNITED

RAIS wa Lazio, Claudio Lotito, amesema Manchester United hawawezi kumsajili kiungo, Sergej Milinkovic-Savic, 27, chini ya pauni milioni 105. ***(Il Messaggero via Mail)***

#### PSG YAMTAJA MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain imekanusha kutumia mlango wa nyuma kufanya kampeni kwenye mitandao ya kijamii dhidi ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 23. ***(Goal)***

#### ATLETICO: FELIX HAUZWI

KLABU ya Atletico Madrid haina mpango wa kumuuza mshambuliaji wao Mreno, Joao Felix, 22, katika dirisha la Januari licha ya nyota huyo kuchukizwa na kusugua benchi. ***(Relevo - in Spanish)***

#### MAGUIRE APIGIWA CHAPUO

KOCHA wa England, Gareth Southgate atamuunga mkono beki wa kati wa Manchester United, Harry Maguire kueleke Kombe la Dunia nchini Qatar, licha ya nyota huyo kuwa na kiwango cha kusuasua. ***(Mirror)***

#### TONEY MAMBO SAFI

KLABU ya Brentford inatazamia kumpa mshambuliaji, Ivan Toney, 26, mkataba mpya ili kukabiliana na Manchester United, Leeds, Newcastle na West Ham zilizoonyesha nia ya kusamjili. ***(Mirror)***

#### TUCHEL AITAMANI ENGLAND

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel anaweza kuvutiwa na mpango wa kukinoa kikosi cha England kama Gareth Southgate ataondoka baada ya Kombe la Dunia la Qatar. Tuchel, 49, amekataa ofa mbili kutoka klabu za Ligi Kuu England tangu atimuliwe Chelsea Septemba, mwaka huu. ***(Telegraph)***

#### EVERTON, IWOBI KUTETA

KLABU ya Everton imeanza mazungumzo ya awali na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Alex Iwobi, 26, kuhusu kumwongeza mkataba mpya. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL SASA AHITAJI KUIFUNDISHA ENGLAND

### Mjerumani huyo azitolea nje klabu mbili kubwa za Ulaya zilizohitaji...

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel angependa kuchukua nafasi ya Gareth Southgate kama Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya England baada ya kumalizika kwa fainali za Kombe la Dunia zinazofanyika mwezi ujao nchini Qatar.

**Kocha huyo wa Ujerumani kwa sasa hana kazi baada ya kutimuliwa kwa mshangao na Chelsea katika mechi sita pekee kutokana na kuanza vibaya kwa msimu wa 2022/23.**

Ilitarajiwa sana jukumu lake lijalo la ukocha litakuwa katika klabu nyingine kubwa Ulaya baada ya kuhusishwa na Juventus.

Lakini kwa mujibu wa gazeti la Telegraph, badala yake anaweza kuingia katika ulimwengu wa usimamizi wa kimataifa, na sio nchi yake.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Tuchel ana nia ya kuchukua jukumu la kuiongoza England baada ya Kombe la Dunia ikiwa nafasi hiyo itapatikana.

Inasemekana muda wa Southgate kuendelea katika nafasi aliyonayo inaelekea kikomo mara baada ya michuano hiyo kukamilika, licha ya mkataba wake unadumu hadi mwaka 2024.

Tayari amekataa nafasi ya kufundisha katika klabu mbili za Ligi Kuu England na moja kutoka nchini Hispania.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,039,5

MECHI KALI
ATHLETIC BILBAO
VERSUS
ATLETICO MADRID
1 | 2.45
X | 3.20
2 | 2.85

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JOAO AOMBA KUONDOKA ATLETICO



**MADRID,** Hispania

JOAO Felix ameomba kuondoka Atletico Madrid katika dirisha dogo la Januari mwakani, kwa mujibu wa ripoti ya Fichajes.


Felix anazidi kuchanganyikiwa na maisha katika klabu hiyo baada ya kuondolewa kwenye kikosi cha kwanza hivi karibuni.

Mreno huyo mwenye umri wa miaka 22 bado hajafunga bao katika Ligi Kuu Hispania (LaLiga) na kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu na hakutumika kama mchezaji wa akiba katikati ya wiki wakati Atletico Madrid ikitoka suluhu na Club Brugge.

Kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amependelea kuwatumia Antoine Griezmann, Alvaro Morata, Matheus Cunha na Angel Correa katika safu ya ushambuliaji.

Fowadi huyo amechanganyikiwa baada ya kuona anatumika kwa kiasi kidogo na hayupo kwenye kikosi cha kwanza tangu kuanza kwa msimu huu.

Mkataba wa Felix unamalizika mwaka 2026 na huenda ikahitaji ada kubwa kumsajili kutoka Atletico Madrid, ambao walilipa euro milioni 126 kwa ajili ya huduma yake mwaka wa 2019.



## *Arteta ataka maboresho zaidi*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anataka kuona maboresho zaidi kutoka kwa Arsenal licha ya kupata ushindi mara sita mfululizo baada ya kushinda bao 1-0 ugenini dhidi ya Bodo/Glimt kwenye Ligi ya Europa, juzi.

Bao la Bukayo Saka lililopatikana dakika ya 24 liliwapa Arsenal ushindi huo, lakini walikumbana na shinikizo kubwa kwenye kipindi cha pili baada ya wenyeji wao kutawala mchezo.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Arteta alikiri timu yake ilihitaji kuendeleza mchezo wao kwa ujumla, licha ya kukiri kuridhika na ushindi waliopata.

"Nimefurahishwa sana na ushindi dhidi ya timu ambayo imeshinda mechi 14 mfululizo nyumbani," alisema kocha huyo raia wa Hispania akiiambia BT Sport.

"Tulitarajia usiku mgumu sana hapa, na tulifanya mabadiliko mengi tena, lakini nina furaha kupata njia ya kushinda. Kufanya hivyo kwa hali yoyote ile ni chanya kwangu na kwa timu.

Saka alifunga mabao manne kwa msimu huu na mshindi wake, lakini Arteta anataka zaidi kutoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.



594,915/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.15/10/22 | 19:00 | Torino vs Juventus | 3.11 | 3.11 | 2.37 |
| 02.15/10/22 | 19:30 | Mallorca vs Sevilla FC | 2.77 | 2.97 | 2.72 |
| 03.15/10/22 | 21:00 | GO Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.89 | 3.29 | 2.41 |
| 04.15/10/22 | 21:45 | Watford vs Norwich City | 2.64 | 3.24 | 2.64 |
| 05.15/10/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.45 | 3.23 | 2.88 |
| 06.15/10/22 | 22:00 | Cambuur vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.39 | 2.60 |
| 07.16/10/22 | 13:15 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 2.33 | 3.44 | 2.89 |
| 08.16/10/22 | 14:30 | Standard Liege vs Royal Antwerp | 2.95 | 3.45 | 2.30 |
| 09.16/10/22 | 15:00 | Celta Vigo vs Real Sociedad | 2.54 | 3.19 | 2.79 |
| 10.16/10/22 | 16:00 | Spezia vs Cremonese | 2.48 | 3.18 | 2.88 |
| 11.16/10/22 | 16:00 | Southampton vs West Ham | 2.79 | 3.38 | 2.44 |
| 12.16/10/22 | 16:00 | Troyes vs AC Ajaccio | 2.25 | 3.13 | 3.28 |
| 13.16/10/22 | 16:00 | Rennes vs Lyon | 2.26 | 3.51 | 2.92 |
| 14.16/10/22 | 17:00 | Hull City vs Birmingham | 2.50 | 3.20 | 2.85 |
| 15.16/10/22 | 17:15 | Real Madrid vs Barcelona | 2.42 | 3.45 | 2.77 |
| 16.16/10/22 | 17:45 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.43 | 3.48 | 2.74 |
| 17.16/10/22 | 18:30 | Union Berlin vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.38 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 15/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4882 | Torpedo Moscow vs Lokomotiv Moscow | 3.76 | 3.61 | 1.86 |
| 14:30 | 2538 | Leicester vs Crystal Palace | 2.22 | 3.36 | 3.01 |
| 15:00 | 4689 | Girona vs Cadiz CF | 1.84 | 3.30 | 4.49 |
| 16:00 | 1114 | Empoli vs Monza | 2.41 | 3.22 | 2.82 |
| 16:30 | 2747 | FC Krasnodar vs Akhmat Grozny | 2.05 | 3.47 | 3.27 |
| 16:30 | 3773 | Werder Bremen vs Mainz | 2.30 | 3.45 | 2.81 |
| 16:30 | 3954 | VfL Wolfsburg vs Monchengladbach | 2.57 | 3.41 | 2.52 |
| 16:30 | 4520 | Eintracht Frankfurt vs Bayer Leverkusen | 2.63 | 3.52 | 2.41 |
| 16:30 | 5912 | Stuttgart vs VfL Bochum | 1.61 | 3.91 | 4.96 |
| 17:00 | 2858 | Fulham vs Bournemouth | 1.81 | 3.63 | 3.98 |
| 17:00 | 3014 | Celtic vs Hibernian | 1.22 | 5.98 | 10.95 |
| 17:00 | 3038 | Volos vs Levadiakos | 1.63 | 3.53 | 5.57 |
| 17:00 | 3595 | Kasimpasa vs Adana Demirspor | 2.98 | 3.43 | 2.23 |
| 17:00 | 3815 | Bohemians vs Sigma Olomouc | 2.22 | 3.38 | 3.18 |
| 17:00 | 4461 | Ross County vs Dundee Utd | 2.34 | 3.14 | 3.04 |
| 17:00 | 4917 | Wolverhampton vs Nottingham | 1.65 | 3.66 | 4.95 |
| 17:00 | 5373 | St Mirren vs Kilmarnock | 2.05 | 3.19 | 3.64 |
| 17:00 | 5673 | Livingston vs St Johnstone | 1.99 | 3.14 | 3.93 |
| 17:15 | 3005 | Valencia vs Elche | 1.41 | 4.60 | 7.00 |
| 18:00 | 2007 | Javor Ivanjica vs Radnicki Nis | 2.36 | 3.16 | 2.77 |
| 18:00 | 2157 | Austria Klagenfurt vs LASK Linz | 3.26 | 3.51 | 1.97 |
| 18:00 | 2886 | Josko Ried vs Rapid Vienna | 3.20 | 3.45 | 2.01 |
| 18:00 | 5288 | Lorient vs Reims | 2.24 | 3.34 | 3.04 |
| 18:30 | 2244 | Sirius FK vs Norrkoping | 2.58 | 3.36 | 2.41 |
| 18:30 | 3851 | IFK Varnamo vs Kalmar | 3.31 | 3.40 | 1.98 |
| 18:30 | 5589 | Kaizer Chiefs vs Chippa Utd | 1.75 | 3.31 | 4.84 |
| 19:00 | 2773 | Genclerbirligi vs Keciorengucu | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 19:00 | 2993 | BATE Borisov vs Dinamo Brest | 1.27 | 5.26 | 8.37 |
| 19:00 | 3067 | Torino vs Juventus | 2.90 | 3.04 | 2.46 |
| 19:00 | 3068 | Altinordu vs Samsunspor | 3.79 | 3.40 | 1.85 |
| 19:00 | 3692 | Dukla Banska Bystrica vs MSK Zilina | 2.72 | 3.41 | 2.28 |
| 19:00 | 5442 | Rosenborg vs Stromsgodset | 1.35 | 5.39 | 6.79 |
| 19:30 | 3949 | Dinamo Moscow vs Gazovik Orenburg | 1.80 | 3.68 | 3.97 |
| 19:30 | 5037 | Tottenham vs Everton | 1.47 | 4.28 | 5.97 |
| 19:30 | 5317 | RB Leipzig vs Hertha BSC | 1.39 | 4.85 | 6.54 |
| 19:30 | 5579 | Mallorca vs Sevilla FC | 2.91 | 3.06 | 2.51 |
| 19:30 | 5873 | Parnu JK Vaprus vs Trans Narva | 4.78 | 4.20 | 1.53 |
| 19:45 | 4087 | Fortuna Sittard vs Waalwick | 2.18 | 3.57 | 2.93 |
| 20:00 | 1568 | Konyaspor vs Gaziantep BB | 1.84 | 3.64 | 3.89 |
| 20:00 | 3079 | Kayserispor vs Galatasaray | 3.88 | 3.58 | 1.86 |
| 20:00 | 5611 | FK Napredak vs Radnik Surduluca | 1.49 | 3.99 | 5.64 |
| 20:05 | 4459 | HNK Gorica vs Hajduk Split | 4.07 | 3.59 | 1.74 |
| 20:15 | 1621 | Bnei Sakhnin vs Maccabi Tel Aviv | 6.03 | 4.18 | 1.44 |
| 21:00 | 3013 | GO Ahead Eagles vs Heerenveen | 2.83 | 3.13 | 2.45 |
| 21:00 | 5896 | Pogon Szczecin vs GKS Piast Gliwice | 1.77 | 3.51 | 3.99 |
| 21:30 | 3884 | FC Winterthur vs Grasshoppers | 2.36 | 3.42 | 2.78 |
| 21:45 | 3470 | Atalanta vs Sassuolo | 1.63 | 3.97 | 4.67 |
| 22:00 | 3763 | Cambuur vs Vitesse Arnhem | 2.54 | 3.43 | 2.54 |
| 22:00 | 4314 | Lens vs Montpellier | 1.41 | 4.67 | 6.56 |
| 22:00 | 5370 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.45 | 3.20 | 2.85 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ASKARI SUMA JKT AJISHINDIA MULTIBET BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa wilaya ya Chamwino, Dodoma, Miraji Sekiko, ambaye ni askari wa Suma JKT ameshinda Sh. milioni 64.2 katika Multibet bonus ya Sportpesa baada ya kucheza mikeka miwili yenye timu 44 kila mkeka mmoja.

**Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za SportPesa jijini, Dar es Salaam, Miraji alisema alianza kucheza na SportPesa kuanzia mwaka jana.**

''Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka 2021 baada ya rafiki yangu wa karibu, Mfaume kuwa anacheza na kushinda mara kwa mara".

Kwa mujibu wa maelezo yake, Miraji alivutiwa na Sportpesa, baada ya kuona washindi walioshinda wanatangazwa kupitia mitandao ya kijamii na magazetini hivyo kumpa moyo na yeye kuamua kujifunza kucheza.

"Mimi nilicheza Multibet bonus ya mechi 44 ambayo niliona naziweza. Unajua nimenunua kidaftari ambacho huwa nachagua timu naziweka na kuanza kuchambua polepole mpaka nikijiridhisha nimezielewa ndio naweka mikeka yangu.

Katika mkeka wangu huu ulioshinda nilichanganya timu za nchi tofauti tofauti kuanzia ligi za madaraja ya chini Brazil, Italia, Ujerumani, Uingereza na nyinginezo". Anasema Miraji

Anamalizia kwa kusema yeye alilenga zaidi timu zenye odds ndogo kabisa kama za kuanzia odds za 1.33, 0.20, 0.11, 0.24 na kuendelea. Mara baada ya kuweka mkeka wake alizifuatilia moja baada ya nyingine mpaka pale timu ya mwisho ilipocheza.

Anamalizia kwa kusema fedha aliyopata kiasi atawekeza kwenye ujenzi wa nyumba yake ambayo tayari alishaanza kuijenga na pia kiasi kingine japo kidogo atatoa fungu la kumi kwa watu ambao anafikiri wanahitaji kushikwa mkono.

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya alimpongeza Miraji kwa ushindi na kuwaasa Watanzania waendelee kuiamini na kucheza na Sportpesa kwani wanaweza kushinda kama Miraji.

Msuya alisema mkeka wa kwanza alishinda Sh milioni 13.6 na bonus yake ikawa Sh. milioni 15 ambayo ilimpa jumla ya Sh. milioni 28.6. Baada ya kodi alibakiwa na Tsh 25,815,119.

Mkeka wa pili alishinda Sh. milioni 16.4 na bonus yake ikawa Sh. milioni 19.7 ambayo ilimpa jumla ya Sh. milioni 36.1 na baada ya kodi alibakiwa na Sh. milioni 32.5




Miraji Sekiko mshindi wa Multibet bonus ya Sportpesa wa Sh. milioni 64.2 akiwa na mfano wa hundi ya kiasi ya alichoshinda. **PICHA: SPORTPESA**

## Kocha Mgunda awaambia Waangola 'SORRY'

INATOKA UKURASA 32

na tahadhari kubwa ili kupata ushindi, tutaingia tukisaka ushindi tu," alisema Mgunda.

Aliongeza kwa sasa wanachokiwaza ni kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa na suala la maandalizi dhidi ya Yanga litafuata baada ya mchezo wa kesho.

"Sasa hivi maandalizi yetu tunayofanya ni ya kuelekea mechi dhidi ya De Agosto, tunataka ushindi, baada ya kufanikiwa lengo hili ndio tutaangalia mechi nyingine," Mgunda alinogeza.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema hoja iliyoibuka hivi karibuni ni namna Simba inavyotakiwa kuzifundisha timu nyingine za Tanzania mbinu za kupata mafanikio katika mashindano ya kimataifa.

# Yanga yafunguka Al Hilal hawaponi

INATOKA UKURASA 32

liwa, wachezaji morali iko juu, viongozi ari iko juu, tunaamini Jumapili Yanga itawakilisha vizuri nchi na Watanzania wote wenye mashaka, wasiwasi na hofu, wataamini Yanga ni timu kubwa ambayo ina uwezo wa kushinda mechi kwenye uwanja wowote ule," Kamwe alisema.

Kiungo, Yusuph Athumani, akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema mawazo na akili zao zimeelekezwa katika kupambana ili kulinda heshima ya klabu yao.

Nyota huyo alisema wamejiandaa kucheza kishujaa kwa ajili ya kupata matokeo mazuri yatakayowapa furaha mashabiki wao na vile vile kuibeba klabu.

"Si kazi nyepesi kwenda kupata matokeo ugenini, ndiyo maana tumejiandaa mara mbili zaidi ya vile tulivyojiandaa mwanzo. Tunawaambia wanachama na mashabiki wetu sisi ni washindani na tunakwenda kupambanana, sisi ni washindi, waamini tunaweza, kikubwa tuwe pamoja, tunaweza kutinga makundi," alisema mchezaji huyo anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 15, 2022

Nipashe




Tuchel sasa aitaka England UKURASA 29



Mashabiki wa Simba walioko Buguruni, Dar es Salaam wakicheza ngoma kwa ajili ya kuhamasisha kujitokeza kwa wingi kuhudhuria mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Premiero De Agosto itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SIMBA SC**

# YANGA YAFUNGUKA AL HILAL HAWAPONI

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## ●●● Yatamba itatinga makundi CAF, hakuna kitakachowazuia kuwamaliza...

MSAFARA wa Yanga wenye watu 52 uliwasili salama Sudan tayari kwa mechi ya marudiano ya hatua ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Al Hilal itakayochezwa kesho saa 3:00 usiku jijini Khartoum, imefahamika.

**Yanga imesafiri ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 waliyoipata dhidi ya wapinzani wao katika mechi ya kwanza iliyochezwa Jumamosi iliyopita hapa nyumbani.**

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi kabla ya kuondoka nchini, Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema kikosi cha timu hiyo kimewafuata Al Hilal huku kukiwa hakuna majeruhi hata mmoja na malengo yao ni kuweka rekodi ya aina yake ya kufuzu hatua ya makundi wakiwa ugenini.

Meneja huyo amesema wamejipanga kuwapa furaha mashabiki wao na wanahitaji wafahamu wamekwenda Sudan kusaka matokeo chanya yatakayowafanya wasonge mbele katika mashindano hayo.

"Maandalizi yanaendelea vizuri, kila kitu kipo vizuri, kocha amefanyia kazi mapungufu ambayo yalijitokeza na ameboresha kila eneo lililokuwa na mapungufu ili tuwe na mchezo bora wa marudiano, kikubwa ni kuomba mashabiki wasikate tamaa, waamini kama tunaweza kuwapa furaha, chochote kwenye mechi ya mpira wa miguu kinawezekana, tunaenda Sudan kupambana ili lengo letu la kwenda makundi litimie." alisema Harrison.

Alisema wanatarajia kushuka katika mechi ya kesho wakiwa na matumaini makubwa huku wakiwa wamejipanga kushangaza wadau kwa kuwapatia furaha waliyokuwa wakiisubiri kwa muda mrefu.

Nassredine Nabi, Kocha Mkuu wa Yanga, aliliambia gazeti hili wamejipanga kupindua meza ili watinge hatua ya makundi ya michuano hiyo na si kwenda kufanya jambo lingine.

Nabi alisema kikosi chake kitakuwa na kazi kubwa ya kuwaondoa wapinzani wao katika mechi hiyo ambayo haitakuwa rahisi huku akisisitiza malengo ya Yanga ni kupambana kutafuta matokeo mazuri.

"Sio mechi rahisi, itakuwa na ushindani mkubwa, tunatakiwa kujipanga vizuri, tayari tumefanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa wapinzani wetu ili kufikia malengo tunayotarajia na Wanayanga," alisema Nabi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema wamechukua tahadhari zote kuelekea mchezo huo wa marudiano ambapo amebainisha wachezaji wana ari na morali kubwa ya kuhakikisha wanapata ushindi na wanasonga mbele.

"Tunajua zimebaki dakika 90 zilizoshikilia safari yetu ya kwenda hatua ya makundi, tumejiandaa na tahadhari zote zimechuku-

INAENDELEA UK. 31

# Mgunda awaambia Waangola 'SORRY'

**Na Saada Akida**

HESABU zimekamilika, hayo ni maneno ya Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema kikosi chake kitaingia na mbinu mpya kuwakabili Premeiro De Agosto katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Simba itawakaribisha mabingwa hao wa Ligi Kuu Angola wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa ugenini wa mabao 3-1 walioupata Jumapili iliyopita huko nchini Angola.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, Mgunda, alisema malengo yao makubwa katika mechi hiyo ni kuona Simba inafuzu hatua ya makundi kwa kupata matokeo mazuri.

Mgunda alisema baada ya kurejea kutoka Angola aliyafanyia marekebisho mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo wa kwanza na hivyo kujipanga kuingia na mbinu tofauti ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuwaondoka Premiero De Agosto.

"Vijana wako tayari, tunahitaji kupata ushindi tu ingawa tunafahamu ubora wa wapinzani wetu, mchezo hautakuwa rahisi kwa sababu Agosto wana timu nzuri na mechi ya kwanza dakika za mwishoni walibadilika," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wote wanatambua umuhimu wa mchezo huo baada ya kila mmoja kufahamu na kukumbuka matokeo machungu ya kuondolewa na Jwaneng Galaxy katika mashindano hayo msimu uliopita.

"Tumejifunza kutokana na makosa, ninaimani na wachezaji wataingia uwanjani wakikumbuka kilichotokea msimu uliopita, tutacheza kwa nidhamu

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >